**OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**DKT: SAADA MKUYA SALUM**
**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO ZANZIBAR**

**JUNI, 2023.**

**YALIYOMO** **UKURASA**


**A. UTANGULIZI .......................................................................................... 1**

**B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS – FEDHA NA MIPANGO .......................................................................................... 2**

**C. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI – MACHI) MWAKA WA FEDHA 2022/2023 .............................................. 3**

*Ukusanyaji wa Mapato*.......................................................................... 3
*Matumizi ya kawaida*.......................................................................... *5*
*Mchanganuo wa Matumizi Kimafungu* .................................................... 5
Fungu F01 (OR-Fedha na Mipango) .......................................................... 5
*Fungu F02 (Mfuko Mkuu wa Serikali)* ...................................................... 9
*Fungu F03 (Tume ya Mipango Zanzibar)* .................................................. 10
*Fungu F04 (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali)* .................................... 13
*Fungu F05 (Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali)* ...................................... 15
*Fungu F06 (Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali)*....................... 17

**D. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO CHINI YA OR- FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI-MACHI 2022/2023 .......................................................................................... 17**

*Programu ya Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRM)*.......................................................................................... 17
*Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)* ........................ 18
*Mradi wa Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)* ............. 18
*Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali* .................................................. 19
*Programu ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)*.......................................................... 19
*Mradi wa Usimamizi wa Kufanya Upembuzi Yakinifu wa Programu na Miradi ya Maendeleo* .......................................................................... 20
*Mradi wa Kupunguza Umasikini kwa Ukuaji wa Uchumi* .......................... 20
*Mradi wa Kuendeleza Takwimu Zanzibar (Statistical Development Project -ZSDP)* .......................................................................................... 20

**E. UTEKELEZAJI WA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA OR-FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI, 2022/2023 ..... 22**

*Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)*..... 22
*Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)*..... 23
*Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)* ..... 24
*Mfuko wa Barabara Zanzibar (ZRF)* ..... 24
*Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA)*..... 25
*Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)*..... 26
*Shirika la Bima (ZIC)* ..... 27

**F. MASHIRIKIANO NA TAASISI NYENGINE ..... 28**

*Wizara ya Fedha na Mipango* ..... 28
*Benki Kuu ya Tanzania*..... 28
*Tume ya Pamoja ya Fedha* ..... 29
*Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania*..... 29

**G. MWELEKEO WA BAJETI YA OR-FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2023-2024 ..... 29**

*Ukusanyaji wa Mapato*..... 29
*Makusanyo ya Fungu F01* ..... 29
*Makusanyo ya Fungu F04* ..... 30
*Makusanyo ya Fungu F05* ..... 30
*Matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo* ..... 31

**H. MWELEKEO WA KAZI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA OR-FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2023/2024 ..... 36**

*Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)*..... 36
*Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)*..... 37
*Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)* ..... 37
*Mfuko wa Barabara (ZRF)*..... 38
*Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)*..... 39
*Shirika la Bima Zanzibar (ZIC)*..... 39
*Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA)* ..... 40

**I.SHUKRANI ..... 41**

**J.HITIMISHO ..... 42**

**VIAMBATISHO ..... 43**

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia neema ya uhai, afya njema na uwezo wa kukutana hapa leo kwa lengo la kujadili Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi) 2022/2023 na Mwelekeo wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa dhamira ya kuendelea kuwatumikia wananchi wote wa Zanzibar.

2. **Mheshimiwa Spika,** pongezi za dhati ziende kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuendelea kuimarisha uchumi, umoja na mshikamano kwa wananchi wote. Kadhalika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wasaidizi wake wakuu; Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa namna wanavyoendelea na majukumu yao ya kumshauri vyema Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

3. **Mheshimiwa Spika,** katika kufanikisha majukumu ya kitaifa kwa ujumla, wananchi tunaridhishwa na uongozi wao, Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa nguvu na ujasiri wa kusimamia majukumu yao yenye lengo na nia madhubuti ya kuleta maendeleo endelevu hapa Zanzibar. Nakushukuru wewe binafsi **Mheshimiwa Spika,** kwa umakini na umahiri wa kuliendesha Baraza la Wawakilishi, pia nawapongeza Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Wenyeviti wa Kamati na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na Watendaji wa Baraza la Wawakilishi, kwa kuendelea kushirikiana na sisi na kutuongoza katika kutekeleza vyema majukumu yetu.

4. **Mheshimiwa Spika**, baada ya shukurani hizo, naomba uniruhusu kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi,2022/2023) na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Taarifa hii imezingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050; Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021 – 2026; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020 – 2025 na Hotuba za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa nyakati mbali

mbali. Bajeti hii pia imezingatia malengo ya Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango 2022-2026.

## B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS – FEDHA NA MIPANGO

5. **Mheshimiwa Spika,** Kibajeti Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango ni Ofisi inayojumuishwa na mafungu makuu sita (6) ndani yake yanaundwa na Idara ishirini na tatu (23), Taasisi saba (7) na Ofisi tano (5) za Pemba.

6. **Mheshimiwa Spika,** OR-Fedha na Mipango inashughulika na masuala ya usimamizi wa Fedha za Umma kwa kutekeleza Majukumu yafuatayo:-

   i. Kusimamia Mapato ya Serikali kutokana na vyanzo mbali mbali vya Mapato yakiwemo Mapato ya Kodi na yasiyokuwa ya Kodi, Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Mikopo ya Ndani (Hati Fungani);

   ii. Kusimamia Mali za Serikali kupitia Usimamizi wa Ununuzi, Utunzaji na Uondoaji wa Mali za Serikali pamoja na Hisa za Serikali katika Mashirika na Kampuni binafsi ambazo Serikali inamiliki;

   iii. Kusimamia Fedha za Umma na Shughuli za Uhasibu na Ukaguzi Serikalini. Katika jukumu hili Ofisi inasimamia Bajeti ya Serikali, usimamizi wa hazina, huduma za uhasibu na ukaguzi wa ndani Serikalini;

   iv. Kusimamia Deni la Taifa kwa kutoa ushauri na kufuatilia mwenendo wa deni la Taifa (Mikopo ya Ndani na Nje) na udhibiti wake;

   v. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera thabiti, mahiri na shirikishi za kodi na fedha;

   vi. Kusimamia maendeleo ya Sekta ya Fedha, inayohusisha masuala ya Benki, Bima, Hifadhi ya Jamii na usimamizi wa Taasisi za Huduma ndogo ndogo za fedha;

   vii. Kusimamia mifumo ya Ukusanyaji na Udhibiti wa fedha za umma;

   viii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa na kuitafsiri kwenye mipango ya kipindi cha muda wa kati kwa kuzingatia idadi ya watu na mahitaji yake;

ix. Kuratibu na kusimamia maendeleo ya uchumi kupitia sekta za Kiuchumi na kijamii;

x. Kuratibu Sera za Kisekta na kupunguza umasikini nchini;

xi. Kusimamia upatikanaji na utoaji wa Takwimu rasmi kwa Maendeleo ya Nchi; na

xii. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mipango ya kitaifa na kimataifa.

## C. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI – MACHI) MWAKA WA FEDHA 2022/2023

7. **Mheshimiwa Spika,** Kabla ya kuwasilisha taarifa ya Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango ya Mwaka 2023/2024, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Muhtasari wa utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi, 2022/2023) kama ifuatavyo:-

8. **Mheshimiwa Spika,** OR- Fedha na Mipango utekelezaji wake umegawika katika maeneo makuu manne, maeneo hayo ni Mapato yanayokusanywa na kusimamiwa na fungu **F01, F04** na **F05**; utekelezaji wa matumizi yanayosimamiwa na **F01, F02, FO3, F04, F05** na **F06**; utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayosimamiwa na OR-Fedha na Mipango na utekelezaji wa Taasisi zilizo chini ya OR-Fedha na Mipango.

***Ukusanyaji wa Mapato***

9. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 2.498 trilioni**, makadirio hayo yalikua ni ongezeko la asilimia **40** ikilinganishwa na makadirio ya **TZS 1.783 trilioni** ya mwaka 2021/2022. Mapato hayo yamejumuisha mapato ya Fungu **F01, F04 na F05.**

10. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai-Machi 2022/23, OR-Fedha na Mipango imekusanya jumla ya **TZS 1.071 trilioni** sawa na asilimia **64** ya makadirio ya kukusanya **TZS 1.671 trilioni** ya kipindi cha tathmini na asilimia **43** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Mgawanyo wa Mapato hayo kimafungu ni kama ifuatavyo:-

i. **F01** imekusanya jumla ya **TZS 956.496 bilioni** sawa na asilimia **69** ya makadirio ya **TZS 1.386 trilioni**;

ii. **F04** imekusanya jumla ya **TZS 39.810 milioni** sawa na asilimia **29** ya makadirio ya **TZS 138.00 milioni**; na

iii. **F05** imekusanya jumla ya **TZS 114 bilioni** sawa na asilimia **40** ya makadirio ya **TZS 284.385 bilioni.**

11. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya OR-Fedha na Mipango yamejumuisha mapato ya kodi ambayo yanakusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa upande wa Zanzibar. Katika kipindi cha Julai – Machi, 2022/2023, mapato yaliyokusanywa na ZRA yamefikia **TZS 449.283 bilioni** sawa na asilimia **97.56** ya makadirio ya kukusanya **TZS 460.499 bilioni**. Makusanyo ya ZRA yameongezeka kwa asilimia **64** ikilinganishwa na makusanyo halisi ya kodi ya miezi tisa ya mwaka 2021/2022 yaliyokua **TZS 274.799 bilioni**. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa upande wa Zanzibar imekusanya jumla ya **TZS 325.611 bilioni** sawa na asilimia **97** ya makadirio ya kukusanya **TZS 337.048 bilioni.** Makusanyo ya TRA yameongezeka kwa asilimia **27** ikilinganishwa na makusanyo halisi ya kodi ya miezi tisa ya mwaka 2021/2022 yaliyokua **TZS 256.921 bilioni**.

12. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mapato yasiyokuwa ya kodi, OR-FM kupitia Fungu **F01** imekusanya jumla ya **TZS 181.601 bilioni** sawa na asilimia **31** ya makadirio ya **TZS 588.700 bilioni** ndani ya kipindi cha tathmini. Kati ya fedha hizo, zimekusanywa jumla ya **TZS 112.831 bilioni** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia **22** ya makadirio ya **TZS 508.473 bilioni,** misaada iliyopatikana ni **TZS 37.165 bilioni** sawa na asilimia **70** ya makadirio ya **TZS 53.325 bilioni** na mikopo **TZS 75.666 bilioni** sawa na asilimia **17** ya makadirio ya kukusanya **TZS 455.149 bilioni** na mapato mengineyo **TZS 68.769 bilioni** sawa na asilimia **86** ya makadirio ya **TZS 80.227 bilioni** ikujumuisha mapato ya uhamiaji na mapato yanayotokana na gawio kutoka Mashirika ya Umma. Kwa upande mwengine, Fungu **F04** imekusanya **TZS 39.81 milioni** sawa na asilimia **29** ya makadirio ya **TZS 138.00 milioni** na Fungu **F05** imekusanya jumla ya **TZS 114 bilioni** sawa na asilimia **40** ya makadirio ya **TZS 284.385 bilioni.**

***Mchanganuo wa mapato unaonekana katika kiambatisho Namba 1***

*Matumizi ya kawaida*

13. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, OR-Fedha na Mipango ilipangiwa kutumia **TZS 660.091 bilioni.** Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya **TZS 173.460 bilioni** zimetumika sawa na asilimia **76** ya makadirio ya **TZS 228.400 bilioni** yaliyopangwa kutumika katika kipindi cha tathmini. Matumizi hayo ni kama yanavyoelezwa hapa chini:

i. Fungu **F01** limetumia **TZS 31.730 bilioni** sawa na asilimia **64** ya makadirio ya **TZS 49.621 bilioni**;

ii. Fungu **F02** limetumia **TZS 119.478 bilioni** sawa na asilimia **86** ya makadirio ya **TZS 138.342 bilioni;**

iii. Fungu **F03** limetumia **TZS 3.019 bilioni** sawa na asilimia **18** ya makadirio ya **TZS 16.424 bilioni**;

iv. Fungu **F04** limetumia **TZS 9.289 bilioni** sawa na asilimia **78** ya makadirio ya **TZS 11.839 bilioni**;

v. Fungu **F05** limetumia **TZS 7.034 bilioni** sawa na asilimia **86** ya makadirio ya **TZS 8.148 bilioni**; na

vi. Fungu **F06** limetumia **TZS 2.910 bilioni** sawa na asilimia **78** ya makadirio ya **TZS 3.752 bilioni.**

*Mchanganuo wa Matumizi Kimafungu*

**Fungu F01 (OR-Fedha na Mipango)**

14. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Fungu **F01**, yamejumuisha programu kuu tatu ndani yake zinajumuisha programu ndogo tisa. Katika kipindi cha Julai-Machi, 2022/2023; Fungu hili limetumia jumla ya **TZS 31.730 bilioni** sawa na asilimia **64** ya makadirio ya kutumia **TZS 49.621 bilioni** ya kipindi hicho na mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

*PF0101-Programu Kuu ya Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Umma*

15. **Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha usimamizi wa mapato na matumizi ya Serikali. Hadi kufikia Machi, 2023; programu hii imetumia jumla ya **TZS 21.311 bilioni** sawa na asilimia **75** ya makadirio ya **TZS 28.298 bilioni.** Programu hii imejumuisha programu ndogo nne ambazo ni:-

i Programu ndogo ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali imetumia jumla ya **TZS 674.907** milioni sawa na asilimia **59** ya makadirio ya **TZS 1.136 bilioni;**

ii Programu ndogo ya Uratibu wa Rasilimali za Nje imetumia **TZS 338.121 milioni** sawa na asilimia **99** ya makadirio ya **TZS 341.849 milioni**;

iii Programu ndogo ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha na Sera za Kodi imetumia **TZS 19.041 bilioni** sawa na asilimia **75** ya makadirio ya **TZS 25.272 bilioni** fedha hizi zimejumuisha na fedha za ruzuku za Taasisi zinazosimamiwa na OR-Fedha na Mipango ambazo ni **TZS 18.707 bilioni** (Mamlaka ya Mapato Zanzibar, ZRA **TZS 11.186 bilioni** na Mfuko wa Barabara, ZRF **TZS 7.521 bilioni**);na

iv Programu ndogo ya Usimamizi wa Mifumo na Udhibiti wa Fedha za Umma imetumia jumla ya **TZS 1.256 bilioni** sawa na asilimia **72** ya makadirio ya **TZS 1.746 bilioni**.

**16. Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu hii kiujumla imetekeleza shughuli zake zikiwemo zifuatazo:-

i. Kuandaa Muongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa Taasisi za Serikali pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwapatia muongozo na maeneo ya mazingatio wakati wa kutayarisha bajeti pamoja na kupokea michango kutoka kwa wadau juu ya kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2023/2024 kupitia Jukwaa la Bajeti na Uchumi;

ii. Kukamilisha Rasimu ya Sheria ya Bajeti. Kwa sasa, Rasimu ya Sheria hiyo imepitiwa na Kamati ya Uongozi ya Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango, na imewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar kwa ajili ya muongozo wa kisheria;

iii. Kuimarika kwa hatua za mageuzi ya mifumo ya kodi, ikiwemo kuratibu Mkutano wa Tathmini ya Mifumo ya Kodi Zanzibar, ambao kwa mara ya kwanza umefanyika hapa Zanzibar;

iv. Kukamilisha Rasimu ya Sheria ya Huduma za Fedha Ndogo Ndogo Zanzibar. Hatua hii, itapunguza au kuondoa changamoto zinazojitokeza kutokana na wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara za huduma za fedha bila ya kufuata taratibu na miongozo ya biashara hapa Zanzibar;

v. Kuendelea na hatua za Uanzishaji na Usimamizi wa Soko la Hisa Zanzibar ambapo hatua iliyofikia ni kumtafuta Mshauri Elekezi ambae ataishauri Serikali juu ya kazi hii. Ofisi imewajengea uwezo watendaji sita (wanawake 2 na wanaume 4) kwa kuwapatia mafunzo ya vitendo kuhusu Masoko ya Mitaji na Dhamana;

vi. Jumla ya maombi 287 ya misamaha ya kodi kutoka taasisi za umma na binafsi yamewasilishwa ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 28.6 ikilinganishwa na kipindi cha Julai-Machi 2021/22 ambapo jumla ya maombi 223 yaliwasilishwa. Kati ya maombi hayo, maombi 174 yenye thamani ya **TZS 65.7 bilioni** yamekubaliwa kutokana na kukidhi masharti ya sheria, na maombi 113 yamekataliwa. Ongezeko la maombi ya misamaha hiyo limetokana na kuongezeka kwa Miradi ya Wawekezaji pamoja na Miradi inayoshirikisha Washirika wa Maendeleo;

vii. Kuratibu upatikanaji wa fedha za mikopo na misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo **Mradi wa Kuboresha Afya ya Mama na Mtoto** *kutoka Benki ya Dunia,* **Mradi wa Ujenzi wa Barabara 3** zenye urefu wa kilomita 103.5 Unguja na Pemba (Kisauni – Fumba, Tunguu – Makunduchi na Mkoani – Chake Chake) na Uwanja wa Ndege Pemba kupitia *UK Export Finance – UKEF;* Miradi ya Uboreshaji wa **Miundombinu ya Elimu ya Msingi na Sekondari (ZIQUIP)** *kupitia Benki ya Dunia;* Mradi wa **Kuwajengea Uwezo Vijana Kujiajiri Kwenye Sekta ya Uchumi wa Buluu (SEBEP)** *kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); na*

viii. Kuratibu pamoja na kukamilisha urejeshwaji wa fedha za Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Terminal III, fedha ambazo awali Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iligharamia jumla ya Dola za Kimarekani 55 milioni ambazo tayari zimerejeshwa kutoka Benki ya Exim ya China ambazo ndizo zitatumika kugharamia Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Mjini Kilomita 100.3.

*PF0102-Programu Kuu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma*

17. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kuwa na mfumo imara wa kusimamia mali za umma na uwekezaji wake. Hadi kufikia Machi, 2023; programu hii imetumia jumla ya **TZS 4.184 bilioni** sawa na asilimia **34** ya makadirio ya **TZS 12.380 bilioni,** fedha hizo zimejumuisha **TZS 499.363 milioni** ikiwa ni malipo ya mishahara, **TZS 57.100 milioni** matumizi ya utekelezaji wa kazi na majukumu ya ofisi, **TZS 1.560 bilioni** zimepelekwa kwa lengo la Hisa za Serikali kwa Shirika la Maendeleo ya Mafuta Zanzibar (ZPDC); **TZS 817 milioni** ikiwa ni malipo ya mwisho ya Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mahakama Kuu, Tunguu, kwa Mkandarasi wa Kampuni ya *Advent Construction* kupitia Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Serikali na **TZS 1.250 bilioni** fedha kwa ajili ya Ruzuku ya Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma (ZPPDA). Programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kufuatilia upatikanaji wa gawio kutoka Mashirika ya Umma ambapo jumla ya **TZS 6.618 bilioni** zilipatikana katika kipindi cha Julai-Machi, 2023 ikiwa ni gawio kutoka Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) **TZS 404.467 milioni**; Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar (ZSTC) **TZS 1.5 bilioni;** Shirika la Bandari **TZS 500 milioni**; Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) **TZS 3.414 bilioni;** na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) **TZS 800 milioni**;

ii. Kufuatilia malipo ya mikataba yatokanayo na majengo ya Serikali yaliyokodishwa ambapo **TZS 213.784 milioni** zimekusanywa;

iii. Kuendelea na zoezi la ukaguzi, uhakiki, tathmini ya Mali za Serikali katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

iv. Kuendelea na zoezi la uondoshaji wa mali chakavu kutoka Taasisi za Serikali ambapo **TZS 920.866 milioni** zimepatikana hadi kufikia Machi, 2023.

*PF0104– Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa OR-Fedha na Mipango*

18. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kuimarisha uendeshaji wa shughuli za Sekta ya Fedha. Hadi kufikia Machi, 2023, programu hii imetumia jumla ya **TZS 6.234 bilioni** sawa na asilimia **64** ya makadirio ya **TZS 9.195 bilioni.** Programu hii imejumuisha Programu Ndogo tatu ambazo ni:-

i. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa OR-Fedha na Mipango hadi kufikia Julai-Machi 2023, imetumia jumla ya **TZS 3.489 bilioni** sawa na asilimia **70** ya makadirio ya **TZS 4.964 bilioni**;

ii. Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti imetumia jumla ya **TZS 1.714 bilioni** sawa na asilimia **80** ya makadirio ya **TZS 2.136 bilioni**. Fedha hizi zimejumuisha na fedha za miradi ya maendeleo **TZS 1.489 bilioni** ikiwemo Mradi wa Uimarishaji Uwezo wa Taasisi katika Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ISP-DRM **TZS 292.785 milioni (Benki ya Maendeleo ya Afrika);** na Progamu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar BIG-Z **TZS 1.196 bilioni (Benki ya Dunia**); na

iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za OR-Fedha na Mipango Pemba, imetumia jumla ya **TZS 1.030 bilioni** sawa na asilimia **54** ya makadirio ya **TZS 1.914 bilioni.**

**19. Mheshimiwa Spika,** Kiujumla Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa OR-Fedha na Mipango imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuimarisha ubora wa takwimu za kifedha kupitia mafunzo kwa wafanyakazi kumi na nane (18) ambapo kati yao wanawake ni wanane na wanaume ni kumi (10). Mafunzo hayo yaliendeshwa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF);

ii. Kuratibu na kuandaa Mpango wa Matumizi ya Muda wa Kati (MTEF) kwa ajili ya matayarisho ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/24;

iii. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini ya OR-Fedha na Mipango; na

iv. Kuratibu mkutano wa kujadili mikakati ya kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato Pemba ambapo wadau 70 kutoka Taasisi za Serikali na sekta binafsi walishiriki na kutoa maoni juu ya njia bora za ukusanyaji na usimamizi wa mapato kwa Mwaka wa Fedha 2023-2024.

***Fungu F02 (Mfuko Mkuu wa Serikali)***

**20. Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Fungu **F02** yanajumuisha Programu Kuu moja ndani yake inajumuisha programu ndogo moja na kutekeleza shughuli zake kama ifuatavyo: -

*PF0201-Programu Kuu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali*

21. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali inayosimamiwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali. Programu hii imetumia **TZS 119.478 bilioni** sawa na asilimia **86** ya makadirio ya **TZS 138.342 bilioni** kwa kipindi cha Julai-Machi 2023, programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Malipo ya marejesho ya Mikopo ya ndani ya Riba ya Hati Fungani **TZS 19.91 bilioni**;

ii. Malipo ya marejesho ya Mikopo ya ndani ya ZSSF **TZS 7.51 bilioni**;

iii. Malipo ya mafao ya Kiinua Mgongo **TZS 16.70 bilioni** kwa wastaafu 740;

iv. Malipo ya Pencheni kwa wastaafu 13,439 wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar **TZS 19.55 bilioni**; na

v. Matumizi mengineyo ya Serikali **TZS 55.81 bilioni**.

*Fungu F03 (Tume ya Mipango Zanzibar)*

22. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Fungu **F03 (Tume ya Mipango)** yanajumuisha **Programu Kuu** tatu ndani yake kuna Programu Ndogo saba (7). Hadi Machi, 2023; Fungu hili limetumia jumla ya **TZS 3.018 bilioni** sawa na asilimia **18** ya makadirio ya kutumia **TZS 16.424 bilioni** ya kipindi cha tathmini yenye mchanganuo wa matumizi kama ifuatavyo:-

*PF0301-Programu Kuu ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi*

23. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kuimarisha uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa na kufanya ufuatiliaji na tathmini wa mipango hiyo. Hadi Machi 2023, programu hii imetumia **TZS 1.146 bilioni** sawa na asilimia **9** ya makadirio ya kutumia **TZS 13.221 bilioni.** Programu hii inajumuisha Programu Ndogo tatu ambazo ni:-

i. Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Kupunguza Umasikini imetumia **TZS 532.235 milioni** sawa na asilimia **5** ya makadirio ya **TZS 11.541 bilioni**;

ii. Programu ndogo ya Uratibu wa Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu imetumia **TZS 306.864 milioni** sawa na asilimia **42** ya makadirio ya **TZS 772.653 milioni**; na

iii. Programu ndogo ya Ufuatiliaji na Tathmini wa Mipango ya Maendeleo imetumia **TZS 307.592 milioni** sawa na asilimia **32** ya makadirio ya **TZS 956.691 milioni**.

**24. Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi imetekeleza shughuli zikiwemo:-

i. Kukamilisha Muongozo wa Uandaaji wa Mpango Mkakati ulioanza kutumika ili kuakisi Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP 2021-2026);

ii. Kukamilisha Muongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Utekelezaji wa ZADEP 2021-2026 na kusambazwa kwa wadau kwa ajili ya matumizi;

iii. Kufuatilia programu na Miradi ya Maendeleo 52 kati ya 72 iliyopangwa sawa na asilimia 60 pamoja na miradi iliyopata fedha za mkopo nafuu wa ahuweni ya UVIKO-19 Unguja na Pemba, ripoti zimeandaliwa na kuwasilishwa Serikalini ili kufahamika hatua zilizofikiwa pamoja na kutatua changamoto zilizojitokeza;

iv. Kuwajengea uwezo maafisa 113 wa Serikali na Wanafunzi wa Skuli 26 za Sekondari juu ya vipaumbele vipya vya kielimu Kitaifa; ambapo maafisa wanawake walikuwa 57 na wanaume 56; na

v. Kukamilisha Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Rasilimali Watu Zanzibar ambayo itatoa muelekeo wa namna gani Serikali itawekeza katika kuimarisha rasilimali watu.

***PF0302-Programu Kuu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Utafiti***

**25. Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kusimamia sera za kiuchumi na kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii kutokana na vipaumbele vya Taifa vya Tafiti zitakazosaidia ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu. Hadi Machi, 2023 programu imetumia jumla ya **TZS 480.791 milioni** sawa na asilimia **40** ya makadirio ya **TZS 1.201 bilioni**. Programu hii inajumuisha programu ndogo mbili ambazo ni:-

i. Programu ndogo ya Ukuzaji wa Uchumi, hadi Machi 2023, imetumia jumla ya **TZS 226.891 milioni** sawa na asilimia **58** ya makadirio ya **TZS 393.862 milioni**; na

ii. Programu ndogo ya Utafiti imetumia jumla ya **TZS 253.900 milioni** sawa na asilimia **31** ya makadirio ya **TZS 807.269 milioni**.

**26. Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Utafiti imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Jumla ya ripoti 14 za kiuchumi zimetolewa, ambazo tisa ni za Mfumuko wa Bei, nne za Mwenendo wa Hali ya Uchumi na moja ya Utabiri wa Hali ya Uchumi nchini kwa miaka mitatu (2022-2025) kwa kutumia Modeli ya Kifedha (financial programming);

ii. Kuandaliwa kwa muhtasari wa sera za kiuchumi na kijamii ili kutoa ushahidi wa kuandaa na kutekeleza sera zikiwemo za uchumi, kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga kwa kutumia mbolea iliyofanyiwa uboreshwaji, ongezeko la thamani la zao la mwani, kupunguza matumizi ya kupikia kuni na kutumia gesi asilia (bioethanol), kilimo mchanganyiko cha mwani na majongoo na mchango wa vikosi vya SMZ katika kukuza uchumi wa vikosi na taifa;

iii. Kuratibu na kukamilisha tafiti tatu (3) zifuatazo:-

   a. Tafiti ya tathmini ya uzalishaji kwa Idara Maalum za SMZ na mchango wake katika ukuaji wa kiuchumi;

   b. Tafiti ya kutathmini hali ya uwezo wa watumishi wa Sekta za Umma Zanzibar; na

   c. Tafiti ya athari za kifafa cha mimba/uzazi kwa wanawake wenye ujauzito.

iv. Matokeo ya tafiti tatu (3) za masuala ya watoto yamewasilishwa Serikalini ili yatumike katika Mipango na maamuzi sahihi zikiwemo Hali Halisi ya Watoto Zanzibar, Uwekezaji wa Nguvu Kazi ya Kesho; na Tathmini ya Hali ya Umasikini Zanzibar.

***PF0303-Programu Kuu ya Uendeshaji na Utumishi wa Tume ya Mipango***

**27. Mheshimiwa Spika,** Lengo la programu hii ni kusimamia shughuli za utendaji na utumishi ndani ya Tume ya Mipango na kuhakikisha kazi zote zinatekelezwa kwa umakini na ufanisi. Hadi Machi, 2023 programu

imetumia jumla ya **TZS 1.391 bilioni** sawa na asilimia **69** ya makadirio ya **TZS 2.002 bilioni**. Programu hii inajumuisha programu ndogo mbili ambazo ni:-

i. Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango imetumia jumla ya **TZS 1.157 bilioni** sawa na asilimia **71** ya makadirio ya **TZS 1.639 bilioni** katika kipindi cha tathmini; na

ii. Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Tume ya Mipango Pemba imetumia jumla ya T**ZS 233.695 milioni** sawa na asilimia **64** ya makadirio ya **TZS 363.228 milioni**.

**28.** **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Uendeshaji na Utumishi wa Tume ya Mipango imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kupatiwa mafunzo kwa wafanyakazi arobaini (40), kati yao ishirini (20) mafunzo ya muda mrefu (wanawake wanane na wanaume 12) na ishirini (20) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi (ambapo wanawake ni 11 na wanaume ni tisa). Lengo la mafunzo haya ni kuimarisha ufanisi katika utendaji wa wafanyakazi.

ii. Mpango Mkakati wa Tume ya Mipango (Strategic Plan 2023-2026) umeandaliwa kwa lengo la kupata muongozo wa utekelezaji wa shughuli zinazoendana na Mipango mikuu ya nchi; na

iii. Kutoa huduma za utawala na uendeshaji zikiwemo usafiri, vifaa vya kuandikia, ununuzi wa vitendea kazi na matengenezo ya Ofisi ili kuimarisha mazingira ya kazi.

***Fungu F04 (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali)***

**29.** **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023, fungu F04 limetumia jumla ya **TZS 9.288 bilioni** sawa na asilimia **78** ya makadirio ya kutumia **TZS 11.839 bilioni** ya kipindi cha tathmini, fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli za Programu kuu zifuatazo:-

***PF0401-Programu Kuu ya Kuendeleza na Kuratibu Takwimu rasmi za Kiuchumi na Kijamii***

**30.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imelenga kuongeza ubora na wingi wa takwimu kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mipango ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Hadi Machi, 2023 programu imetumia **TZS 7.253 bilioni** sawa na asilimia **76** ya makadirio ya **TZS 9.533 bilioni** kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kukusanya, kuchakata, kukamilisha na kutoa ripoti mbali mbali za kitakwimu za kila mwezi na robo mwaka na kusambazwa kwa wadau kwa njia ya Tovuti, Machapisho na Vyombo vya Habari; Hadi Machi 2023, jumla ya ripoti 16 za kila mwezi na robo mwaka zimetolewa. Ripoti hizo zinajumuisha; Takwimu za Faharisi ya Bei ya Mlaji, Takwimu za Wageni Wanaoingia Nchini na Takwimu za Pato la Taifa, Takwimu za matukio ya Ajali na Makosa Barabarani, Ripoti ya Takwimu za Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto pamoja na Takwimu za Biashara;

ii. Kusimamia shughuli za tafiti Zanzibar kwa kutoa ushauri wa kitaalamu na kutoa vibali vya kuendesha tafiti hizo. Hadi Machi 2023, jumla ya vibali 201 vimetolewa (wazawa 185 na wageni 16) ambapo vibali 182 kwa wanafunzi, vibali 13 vilitolewa kwa Taasisi na vibali 6 vilitolewa kwa mahitaji mengine;

iii. Kutoa ushauri na msaada wa kiufundi kwa wazalishaji na watumiaji wa takwimu za kiuchumi juu ya mfumo wa ukadiriaji wa Uchumi na kufanya makadirio ya hali ya ukuaji wa Uchumi kwa miaka ijayo; na

iv. Kukamilisha ripoti ya utafiti juu ya Sensa na Tafiti za Kijamii utafiti ambao hufanyika kila mwaka.

***PF0402-Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali***

31. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Utawala na Uendeshaji imejumuisha programu ndogo mbili (2) ikiwemo Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji Unguja pamoja na Uratibu wa shughuli za kitakwimu Pemba. Hadi Machi 2023, Programu imetumia jumla ya **TZS 2.034 bilioni** sawa na asilimia **88** ya makadirio ya **TZS 2.306 bilioni**. Fedha hizo zilitumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Matumizi ya uendeshaji wa ofisi yamefanyika ikiwemo ununuzi wa vitendea kazi; na

ii. Kuendelea kukamilisha mpango wa mafunzo wa miaka mitano (5) kupitia Programu ya Uendelezaji Takwimu kwa lengo la kujenga uwezo kwa ofisi pamoja na sekta kitakwimu.

*Fungu F05 (Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali)*

32. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali hadi Machi 2023, imetumia **TZS 7.034 bilioni** sawa na asilimia **86** ya makadirio ya **TZS 8.147 bilioni** ya kipindi cha tathmini, fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli za Programu kuu zifuatazo:-

*PF0501- Programu Kuu ya Usimamizi wa Hazina*

33. **Mheshimiwa Spika,** Hadi Machi 2023, programu hii imetumia jumla ya **TZS 241.582 milioni** sawa na asilimia **37** ya makadirio ya **TZS 645.103 milioni** kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kufanyika kwa mapitio ya vyanzo vya mapato yasiyokua ya kodi kutoka taasisi mbali mbali za Serikali na Usimamiaji wa ufanyaji wa usuluhishi wa mapato;
ii. Kupatiwa mafunzo ya kitaalamu juu ya usimamizi na usalama wa mifumo ya usimamizi wa fedha ambayo yamesaidia kuimarisha usalama wa taarifa zilizopo katika mfumo;
iii. Uhakiki kwa wastaafu wanaolipwa stahiki zao na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umefanyika, kazi ambayo imesaidia kuimarisha taarifa za wastaafu;
iv. Kupatiwa mafunzo ya usimamizi wa Mfumo Mpya wa Usimamizi wa Madeni (CS Meridian), mfumo ambao utasaidia uwekaji wa taarifa za madeni kielekroniki; na
v. Kutoa ushauri wa mikopo kwa uandaaji wa vikao vya Kamati ya Deni la Taifa, vinavyoishauri Serikali kutokana na maombi ya mikopo, mwenendo mzima wa Deni la Taifa na athari za deni kwa uchumi.

*PF0502- Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali*

34. **Mheshimiwa Spika,** Hadi Machi 2023, programu hii imetumia jumla ya **TZS 6.792 bilioni** sawa na asilimia **91** ya makadirio ya **TZS 7.502 bilioni** kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Malipo ya mishahara pamoja na stahiki mbali mbali za wafanyakazi;

ii. Kuwawezesha wahasibu 27 wa Serikali kushiriki katika mafunzo ya kitaalamu katika Fani ya Uhasibu (CPA) ambapo wahasibu wanawake 14 na wahasibu wanaume 13 walishiriki; na

iii. Kununua vitendea kazi vya Ofisi kwa lengo la kuimarisha utendaji na ufanisi.

***Fungu F06 (Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali)***

35. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali hadi Machi 2023, imetumia **TZS 2.910 bilioni** sawa na asilimia **78** ya makadirio ya **TZS 3.752 bilioni** kwa programu kuu mbili. Matumizi ya fedha kiprogramu ni kama ifuatavyo:-

***PF0601-Programu Kuu ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani Serikalini***

36. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya kusimamia ukaguzi wa ndani Serikalini imejumuisha programu ndogo tatu (3) ikiwemo Programu ya usimamizi wa kamati za ukaguzi na taarifa jumuishi za ukaguzi wa ndani, Programu ndogo ya uchunguzi wa ubadhirifu na vihatarishi na Programu ndogo ya usimamizi wa uthibitisho wa ubora. Hadi Machi 2023, programu imetumia jumla ya **TZS 211.310 milioni** sawa asilimia **23** ya makadirio ya **TZS 909.860 milioni** kwa kutekeleza pamoja na shughuli nyengine, kazi zifuatazo:-

i. Ufuatiliaji wa ubora wa kazi za ukaguzi wa ndani umefanyika kwa kuangalia utekelezaji wa mipango ya ukaguzi kwa mwaka, katika Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

ii. Kaguzi maalum kumi na tano (15) zimefanyika kwa Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali zikiwemo, Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Shirika la Umeme Zanzibar, Mamlaka ya Mapato Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar, Mabaraza ya Manispaa, Mabaraza ya Miji, Halmashauri pamoja na Mamlaka ya Uendeshaji na Uhifadhi wa Mji Mkongwe kwa lengo la kuongeza udhibiti wa ndani wa fedha na kuibua viashiria vya ubadhirifu wa kifedha; Tayari taarifa juu ukaguzi huu imekamilika na itawasilishwa Serikalini kwa hatua stahiki;

iii. Kuandaa Taarifa Jumuishi ya Ukaguzi wa Ndani za Wizara na Taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na

iv. Mafunzo ya “Performance Audit Technique” yametolewa kwa Wakaguzi Wakuu wa ndani 45 wa Unguja na Pemba juu ya masuala ya manunuzi, usimamizi wa mikataba pamoja na usimamizi wa miradi kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa kazi za ukaguzi.

***PF0601- Programu Kuu ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani Serikalini***

**37.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Utawala na Uendeshaji imejumuisha programu ndogo mbili (2) ikiwemo programu ndogo ya Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mipango, Mafunzo na Utafiti na Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi Pemba. Hadi Machi 2023, programu imetumia jumla ya **TZS 2.699 bilioni** sawa asilimia **95** ya makadirio ya **TZS 2.843 bilioni.** Fedha hizo zilitumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kushiriki mikutano ya Washirika wa Maendeleo wakiwemo Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa lengo la kujenga uwezo wa watendaji wa Ofisi katika masuala ya ukaguzi;

ii. Kukamilisha Rasimu ya Sheria ya Ukaguzi wa Ndani kwa lengo la kutoa muongozo wa ukaguzi wa ndani na uendeshaji wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani; na

iii. Kupatiwa mafunzo ya “Risk Based Internal Audit” kwa Wakaguzi Wakuu wa Ndani 20 yaliyoimarisha ukaguzi kwa kuangalia maeneo hatarishi kupitia Benki Kuu ya Tanzania na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan.

***Mchanganuo wa matumizi unaonekana katika kiambatisho Namba 2***

## D. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO CHINI YA OR-FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI-MACHI 2022/2023

***Programu ya Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRM)***

**38.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ina lengo la kuimarisha rasilimali za ndani na usimamizi wa maliasili. Hadi Machi 2023, Programu hii imetumia **TZS 292.785 milioni** sawa na asilimia **20** ya makadirio ya **TZS 1.46 bilioni** ya mwaka na kutekeleza shughuli ikiwemo utoaji wa mafunzo wa namna ya kutathimini na kufuatilia mapato yatokanayo

na mafuta na gesi kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Kitengo cha Tehama cha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar juu ya usimamizi na usalama wa mfumo (CEHv 10) pamoja na taarifa pamoja na gharama za uendeshaji wa Ofisi ya mradi.

***Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)***

39. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar ina lengo la kuimarisha hali ya maisha na kukuza Maendeleo ya kiuchumi Zanzibar katika utoaji wa huduma, uhifadhi wa urithi na usimamizi jumuishi wa Miji. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, mradi huu umekadiriwa kutumia **TZS 47.13 bilioni**. Hadi Machi 2023, jumla ya **TZS 1.196 bilioni** sawa na asilimia **3** zimetumika kwa kuendelea kukamilisha Zabuni za miradi ambazo ziko katika hatua tofauti, mradi unaendelea kukamilisha Zabuni ikiwemo ya kupata wataalamu wa kutoa huduma za kitaalamu na ujenzi wa maeneo ya miradi.

40. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia kuwa kazi kubwa za mradi zinazoendelea ni taratibu za ununuzi wa kupata washauri elekezi wa kubuni na kusanifu kazi za ujenzi na kupelekea kasi ndogo ya matumizi ya fedha za mradi ambazo kwa kiasi kikubwa zimetengwa kwa ajili ya kazi za ujenzi.

***Mradi wa Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)***

41. **Mheshimiwa Spika,** Lengo la Programu hii ni kuimarisha Usimamizi wa Fedha za Umma. Programu hii inatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na washirika wa maendeleo ambao ni *Norway, DfID na Denmark*. Hivyo, Programu hii inahakikisha mapato na matumizi yanasimamiwa na kudhibitiwa kwa ufanisi mkubwa katika taasisi za Serikali.

42. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Programu hii umeimarisha utendaji kazi kwa kupata vitendea kazi, mifumo ya kielektroniki na ujuzi kwa wafanyakazi na hatimaye kuimarisha usimamizi mzuri wa Fedha za Umma. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Programu imepangiwa jumla ya **TZS 3.7 bilioni**. Hata hivyo, fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo hazijapatikana kutokana na mabadiliko ya utaratibu wa fedha hizo kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa sasa, majadiliano yanaendelea baina ya Washirika wa Maendeleo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

*Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali*

43. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuweka mazingira bora ya kazi ili kuimarisha ufanisi katika kutoa huduma stahiki kwa wananchi. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 programu imepangiwa **TZS 92 bilioni** kwa ujenzi wa Ofisi za Serikali. Hadi Machi 2023, programu imetumia **TZS 817.00 milioni** sawa na asilimia **1** kwa ajili ya malipo ya mwisho ya Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mahakama Kuu ya Tunguu iliyolipwa kwa kampuni ya *Advent Construction.*

44. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi tayari imeshaandaa eneo la Ujenzi wa Mji wa Serikali limeshapatikana ambalo ni Kisakasaka. Hati za umiliki wa eneo hili tayari zimeshaandaliwa na ukamilishaji wa Ramani unaendelea. Matarajio ni kuwa kazi za ujenzi wa mradi wa Mji wa Serikali kuanza rasmi katika mwaka wa fedha 2023/24.

*Programu ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)*

45. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imelenga kuwakwamua wananchi na umasikini kupitia urasimishaji wa biashara na ardhi ili ziweze kutumika katika kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka 2022/2023, mradi huu umekadiriwa kutumia jumla ya **TZS 4.5 bilioni.** Hadi Machi 2023, programu hii imetumia **TZS 307 milioni** kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sawa na asilimia **8.5** ya makadirio ya **TZS 3.6 bilioni** (**TZS 3.1 bilioni** kutoka SMZ na **TZS 500 milioni** kutoka SMT) na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kufanyika kwa mikutano ya uhamasishaji wa urasimishaji wa ardhi na biashara kwa wananchi wa shehia ya Meya, Mwanakwerekwe, Mkokotoni, Donge na Mwera juu ya umuhimu wa kurasimisha ardhi na Biashara ili ziweze kuinua vipato vyao;

ii. Kutambuliwa na kusajiliwa jumla ya Viwanja 1,680 (Gombani 290, Konde 310, Meya 868 Jambiani 212) na kutoa hati 193 kwa wananchi (127 Unguja na 66 Pemba); na

iii. Kujengwa Jengo la Masjala ya Ardhi Mwanakwerekwe na Kituo Jumuishi cha Urasimishaji Biashara Wilaya ya Chake Chake Pemba.

*Mradi wa Usimamizi wa Kufanya Upembuzi Yakinifu wa Programu na Miradi ya Maendeleo*

46. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalenga kufanya uratibu na usimamizi wa uandaaji wa upembuzi yakinifu na Mapitio ya Sekta kijamii na kiuchumi. Hadi Machi 2023 mradi ulikadiriwa kutumia **TZS 6.739 bilioni,** hakuna fedha iliyopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi huo. Hata hivyo, sekta zimeendelea kusimamia Upembuzi Yakinifu kwa Miradi yao inayohitaji kutekelezwa kwa taratibu mbali mbali.

*Mradi wa Kupunguza Umasikini kwa Ukuaji wa Uchumi*

47. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalenga kufanya tafiti ndogo kwa shehia zilizoripotiwa kuwa na umasikini kutokana na ripoti ya matumizi ya kaya HBS kwa lengo la kuja na mbinu mbali mbali ikiwemo miradi midogo midogo ya wananchi ya kupunguza umasikini. Kwa kipindi cha Julai-Machi 2023, mradi umekadiriwa kutumia **TZS 761.250 milioni**, hakuna fedha iliyopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi. Hata hivyo, baadhi ya shughuli zimefanyika ikiwemo vipindi viwili vya Redio na vitatu vya Televisheni kuzungumzia juhudi za Serikali katika kupambana na Umasikini Zanzibar ikiwa maadhimisho ya Wiki ya Kupambana na Umasikini Duniani ambayo huadhimishwa kuanzia tarehe 13-19 Oktoba kila mwaka Duniani kote.

*Mradi wa Kuendeleza Takwimu Zanzibar (Statistical Development Project -ZSDP)*

48. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu umelenga kuimarisha shughuli za kitakwimu Zanzibar ikiwemo kuwezesha ukusanyaji, upatikanaji na utoaji wa takwimu za kawaida kwa wakati; kuweka mazingira mazuri ya kuratibu upatikanaji wa viashiria na takwimu za Kiuchumi na Kijamii kupitia takwimu za kawaida, Sensa na tafiti kwa ajili ya uandaaji, ufuatiliaji na kufanya tathmini ya utekelezaji wa ajenda na Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, kikanda na kimataifa, pamoja na kujengea uwezo wa Watumishi wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

49. **Mheshimiwa Spika,** Hadi Machi 2023, mradi umetumia jumla ya **TZS 7.09 bilioni** sawa na asilimia **75** ya makadirio ya **TZS 9.43 bilioni** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

**i. Zoezi la Sensa ya Watu na Makaazi**

**50. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu Tanzania (NBS) baada ya uzinduzi wa matokeo ya awali zimekamilisha na kuwasilisha ripoti mbali mbali zikiwemo ripoti ya Kiutawala ambayo inajumuisha Idadi ya Watu Kimikoa, Kiwilaya na Shehia, Ripoti ya Mgawanyo wa Watu Kiumri na Kijinsia, Ripoti ya Mgawanyo wa Watu katika Majimbo pamoja na ripoti ya matokeo muhimu ya Kiumri na Kijinsia.

**ii. Utafiti wa Viashiria na matokeo ya Ukimwi (Tanzania HIV Impact Survey -THIS).**

**51. Mheshimiwa Spika,** Utafiti huu una lengo la kujua hali ya ukubwa wa maambukizi ya VVU na Homa ya Ini B na C nchini pamoja na Viashiria vyake. Hadi Machi 2023, kazi ya kukusanya taarifa za kaya imekamilika Unguja na Pemba na jumla ya Kaya 4,000 zimehojiwa katika utafiti. Matokeo ya utafiti huu, yatatangazwa mara baada ya kazi ya tathmini kukamilika.

**iii. Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria (TDHS/MIS)**

**52. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) imekamilisha uwasilishaji wa ripoti ya Utafiti kwa wadau kwa ajili ya matumizi.

**iv. Mpango Kabambe wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II)**

**53. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu Tanzania (TSMPII) unatekelezeka kwa ufanisi NBS na OCGS kwa kushirikiana na Benki ya Dunia ziliratibu mafunzo kwa waratibu wa mradi pamoja na kuandaa bajeti za utekelezaji wa mradi kwa kila shughuli iliyopangwa kupitia mradi huo kwa kuwashirikisha wahusika wa shughuli hizo.

**v. Programu zilizo Chini ya Mfuko wa Pamoja**

**54. Mheshimiwa Spika,** Kupitia programu ya "European Union Trust Fund" (EUTF) na UNFPA, Ofisi inaendelea na kazi ya uchambuzi na uandaaji wa ripoti ya utafiti wa kuangalia ustawi wa kaya kwa vipindi vifupi kwa mwaka 2022 (high frequency welfare monitoring phone survey 2022) ambapo watendaji wa NBS na OCGS wameshiriki kufanikisha kazi hiyo.

### vi. Uwasilishaji wa Ripoti ya Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi

55. **Mheshimiwa Spika,** Ripoti ya Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanya Kazi ya mwaka 2020/21 inaonyesha ongezeko la idadi ya wasiokuwa na ajira imefikia asilimia 19.6 ikilinganishwa na asilimia 14.3 ya mwaka 2014. Kwa mujibu wa matokeo hayo imeonekana kuwa Mkoa wa Mjini Magharibi unaongoza kwa kuwa na ongezeko la ukosefu wa ajira kwa asilimia 26.6 kwa mwaka 2020/21 kutoka asilimia 23.1 ya mwaka 2014. Aidha, utafiti umebaini kuwa katika Mkoa wa Kusini Unguja na Kusini Pemba, tatizo la ukosefu wa ajira limepanda kwa kasi kubwa ambapo Mkoa wa kusini Unguja umepanda kwa asilimia 12.5 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na asilimia 3.9 ya mwaka 2014, na Mkoa wa Kusini Pemba ongezeko la ukosefu wa ajira limepanda kutoka asilimia 6.9 ya mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 14.0 ya mwaka 2020/21.

### vii. Utafiti wa Kufuatilia Kaya (National Panel Survey)

56. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa Kushirikiana na NBS imekamilisha Utafiti wa Kufuatilia Kaya (NPS) ambapo kwa upande wa Zanzibar, matokeo yanaonyesha idadi ya akina mama waliohudumiwa na wataalamu wa afya wakati wa kujifungua imeongezeka kutoka asilimia 66.3 mwaka 2014/15 hadi asilimia 85.6 mwaka 2020/21. Kumekuwa pia na ongezeko katika idadi ya watu walioelezea kuridhishwa na huduma za afya walizopatiwa pindi walipofika katika vituo vinavyotoa huduma za afya.

## E. UTEKELEZAJI WA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA OR-FEDHA NA MIPANGO KWA KIPINDI CHA JULAI -MACHI, 2022/2023

### *Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)*

57. **Mheshimiwa Spika,** Katika Kipindi cha Julai hadi Machi 2023, Mamlaka ya Mapato Zanzibar, ZRA ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 460.499 bilioni** na imeweza kukusanya jumla ya **TZS 449.283 bilioni** ambazo ni sawa na asilimia **97.56** ya makadidirio. Kwa kulinganisha na makusanyo ya kipindi kama hiki kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 kuna ongezeko la makusanyo halisi ya **TZS 274.799 bilioni** sawa na ukuaji wa asilimia **63.50**. Ongezeko hili limetokana na kuendelea vizuri kwa kasi ya ukuaji wa uchumi na wageni walioingia nchini ikiwa pamoja na:-

i. Kuimarika huduma kwa walipakodi; Mamlaka imeendelea kuimarisha huduma za kikodi kupitia ofisi zake za Mikoa ya Kodi ya Unguja na Pemba. Aidha, kiwango cha utolewaji wa elimu ya kodi kupitia semina, mikutano na walipa kodi, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ikiwemo *ZRA ONLINE TV*, vimeongeza ulipaji kodi wa hiari kwa kiasi kikubwa;

ii. Matumizi ya mifumo katika ukusanyaji wa kodi, usimamizi wa matumizi ya mfumo wa kutolea risiti za kielektroniki (VFMS), pamoja na uimara na upatikanaji kwa wakati wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ndani ya Mamlaka imechangia ukusanyaji mzuri wa mapato;

iii. Uweledi na uadilifu kwa wafanyakazi; kuendelea kuwajengea uwezo watendaji wa Mamlaka kuweza kutoa huduma bora zaidi kwa walipakodi, pamoja na Kuimarika kwa viwango vya uadilifu wao, vimesaidia kufikia ufanisi; na

iv. Uwajibikaji wa Hiari wa walipa kodi kwa baadhi ya Walipa kodi, umechangia sana ufanisi wa kiwango kilichofikiwa. Aidha, kutowajibika kulipa kodi kwa hiari kwa baadhi ya walipa kodi, ikiwemo kutotoa risiti za kielektroniki (VFD), kumechangia kutofika Ufanisi wa asilimia 100.

***Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)***

58. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023, imekusanya jumla ya **TZS 325.611 bilioni** ya makadirio ya **TZS 337.048 bilioni** sawa na asilimia **97** ya makadirio ya kipindi hicho cha tathmini.

59. **Mheshimiwa Spika,** katika mapato halisi yaliyokusanywa, Idara ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa ilikusanya **TZS 156.859 billioni** na Idara ya Kodi za Ndani ilikusanya **TZS 168.752 billioni**. Jumla ya Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar katika kipindi kama hicho mwaka uliopita ni **TZS 325.611 bilioni**, ambayo ni sawa na ongezeko la **TZS 68.319 bilioni** sawa na asilimia **27**.

60. **Mheshimiwa Spika,** Changamoto zinazoikabili Mamlaka ya Mapato Tanzania katika ukusanyaji wa mapato ikiwemo ufinyu na miundombinu isiyo ridhisha kwa Bandari ya Zanzibar bado imekua changamoto na kupelekea ucheleweshwaji wa mizigo pamoja na kodi za Serikali na kuwepo kwa idadi kubwa ya biashara zisizo rasmi. Aidha, kupungua kwa

uingizaji wa baadhi ya bidhaa kama sukari, mafuta na saruji kutokana na mabadiliko ya sheria yaliyofanyika kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

61. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Tanzania imejiwekea mikakati ikiwemko kuweka mkazo zaidi katika kuwafikia walipa kodi zaidi pamoja na kuongeza usimamizi wa ukaguzi, ufuatiliaji wa madeni na udhibiti wa bidhaa zinazoingia nchini ili kufikia malengo ya ukusanyaji yaliyowekwa pamoja na kuongeza umakini katika ukaguzi wa ritani zinazowasilishwa na walipa kodi.

***Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)***

62. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Benki ya Watu wa Zanzibar PBZ, ilifanikiwa kupata faida ya jumla ya **TZS 42 bilioni** kulinganisha na kiwango kilichokadiriwa cha **TZS 32 bilioni** ambayo ni asilimia **132** ya makadirio. Hadi Machi, 2023 benki ina jumla ya rasilimali (Assets) **TZS 1,547 bilioni** ukilinganisha na **TZS 1,062 bilioni** kwa mwezi wa Machi 2022 ambalo ni ongezeko la asilimia **46** na kufanikiwa kuingia katika kundi la mabenki makubwa Tanzania.

63. **Mheshimiwa Spika,** Amana za wateja zimeongezeka kufikia **TZS 1,111 bilioni** katika mwezi wa Machi, 2023 sawa na asilimia **26** kutoka **TZS 881 bilioni** mwezi wa Machi 2022. Aidha, Mtaji wa benki hadi Machi 2023, ni **TZS 159 bilioni** ni ongezeko la asilimia **25** kutoka Machi, 2022 **(TZS. 127 bilioni).** Hadi Machi 2023, mikopo kutoka sekta tofauti imekuwa kwa asilimia **40** kutoka **TZS 628,668 milioni** kwa mwezi wa Julai-Machi 2022 hadi **TZS 881,103 milioni** kwa mwezi wa Julai-Machi 2023.

64. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 benki ilitarajia kupata mapato kutoka vyanzo vyake vya riba na visivyo na riba kwa **TZS 92,866 milioni** na ikafanikiwa kupata mapato ya **TZS 105,308 milioni** ambayo ni sawa na asilimia **113** ya lengo, kuongezeka kwa mapato kumetokana na kuongezeka kwa mapato ya riba na mapato yasio na riba.

***Mfuko wa Barabara Zanzibar (ZRF)***

65. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, ZRF iliidhinishiwa jumla ya **TZS 22.168 bilioni** ambapo **TZS 21.775 bilioni** ni matumizi ya kawaida na **TZS 392.6 milioni** malipo ya mishahara.

Asilimia **92** ya fedha za matumizi ya kawaida sawa na **TZS 20.033 bilioni** zilipangwa kwa utunzaji na matengenezo ya barabara. Hadi Machi 2023, fedha zilizopatikana ni **TZS 7.519 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 3.600 bilioni** zimetumika ambapo **TZS 2.877 bilioni** zililipwa kwa kazi za utunzaji na matengenezo ya barabara zinazotekelezwa na Wakala wa Barabara Zanzibar na kutumika kwa Matengenezo ya kawaida kwa Unguja na Pemba, kuziba viraka, kuendeleza matengenezo makubwa ya barabara ya Kipapo–Mgelema-Wambaa pamoja na matengenezo ya mtaro wa kuondosha maji ya mvua yanayofurika eneo la makutano ya barabara ya Mfenesini-Bumbwini. Aidha kazi za uendeshaji Ofisi na kujenga uwezo kwa watendaji wa ZANROADS.

66. **Mheshimiwa Spika,** ZRF imeendeleza na kazi za mapitio ya nyaraka mbali mbali za kiutendaji kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuimarisha utendaji nyaraka za miongozo na mapendekezo zimetayarishwa zikiwemo Kanuni za Fedha, Mpango Mkakati 2023/2024 – 2025/2026, Miongozo ya Bodi na Kamati zake na mapendekezo ya taratibu za utumiaji na utunzaji wa barabara.

***Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA)***

67. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ZPPDA, imekadiriwa kukusanya **TZS 456 milioni** kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato ikiwemo usajili wa watoa huduma, mafunzo ya mpango wa manunuzi, ada ya nyaraka za zabuni na matangazo ya zabuni. Hadi Machi 2023, Mamlaka imekusanya **TZS 323 milioni** sawa na asilimia **71** ya makadirio.

68. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, hadi Machi 2023, Mamlaka imetumia jumla ya **TZS 1.250 bilioni** sawa na asilimia **54** ya kupokea ruzuku ya **TZS 2.317 bilioni** kwa mwaka**,** kati ya Fedha hizo **TZS 798.477 milioni** kwa ajili ya Mishahara na **TZS 451.976 milioni** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kukagua Taasisi nunuzi 30 Unguja na Pemba kwa lengo la kuhakikisha usimamiaji na utumiaji wa Sheria ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, namba 11 ya mwaka 2016 unatekelezwa ipasavyo;

ii. Kufanya kikao na Maafisa manunuzi 84 juu ya kujadili mafanikio na changamoto zinazowakabili wakati wa utekelezaji wa majukumu yao sambamba na matumizi ya mfumo;

iii. Mamlaka imeendelea kutoa mafunzo ya mfumo wa ununuzi wa mtandao (*e-Proz*) kwa Bodi ya Zabuni na watendaji wa ununuzi kwa Taasisi nunuzi 45 kwa awamu ya kwanza na Taasisi 55 kwa awamu ya pili na watoa huduma 321 kwa upande wa Unguja na Taasisi 54 na Watoa Huduma 221 kwa upande wa Pemba. Aidha kufanyika kikao cha pamoja na Maafisa manunuzi 84 kwa ajili ya kujadili mafanikio na changamoto zinazowakabili wakati wa utekelezaji wa majukumu yao sambamba na matumizi ya mfumo; na

iv. Mamlaka imesajili watoa huduma 1,822 kwa kupitia mfumo wa ununuzi wa mtandao (*e-Proz)*.

***Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)***

**69. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai-Machi 2023 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ZSSF, umekadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 44.540 bilioni** katika uwekezaji na umefanikiwa kukusanya **TZS 45.399 bilioni** sawa na asilimia **102**. Mapato ya Mfuko kutokana na uwekezaji katika kipindi cha Julai 2022-Machi 2023 yalifikia **TZS 45.399 bilioni** ukilinganisha na mapato yaliyopatikana kwa kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, Mapato yameongezeka kwa kiasi cha **TZS 3.703 bilioni** ambayo ni ongezeko la asilimia **8**.

**70. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai - Machi 2023, ZSSF imekusanya michango jumla ya **TZS 97.280 bilioni** sawa na asilimia **118** ya makadirio ya **TZS 82.390 bilioni**. Kwa kipindi kama hichi Julai 2021 - Machi 2022 kulikuwa na lengo la kukusanya michango **TZS 69.434 bilioni** Michango iliyokusanywa ni jumla ya **TZS. 69.816 bilioni** ikiwa ni sawa na asilimia **101**. Aidha, Mfuko katika kipindi cha Julai-Machi 2023, ulipanga kukusanya michango kutokana na Mfuko wa Hiari jumla ya **TZS 340 bilioni** Michango iliyokusanywa ni **TZS 333.361 bilioni** ikiwa ni sawa na asilimia **98**.

**71. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai - Machi 2023, ZSSF ilitarajia kulipa mafao ya uzeeni (kiinua mgongo) kwa wanachama **1,440** kwa **TZS 19.586 bilioni** Jumla ya wanachama **866** wamelipwa mafao na jumla ya **TZS 17.748 bilioni** zimetumika. Aidha, ZSSF ilitarajia kulipa mafao ya uzazi kwa wanachama **1,159** kwa **TZS 214.589 bilioni** Jumla ya wanachama **984** wamelipwa mafao na jumla ya **TZS 210.985 bilioni** zimetumika. Aidha, Penchenia **10,790** walitarajiwa kulipwa pencheni zao kwa **TZS. 13.716 bilioni** Wastaafu **11,620** wamelipwa pencheni zao na jumla **TZS 17.159 bilioni** zilitumika.

72. **Mheshimiwa Spika,** Thamani ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar hadi kufikia Machi 2023 imefikia jumla ya **TZS. 782.179 bilioni** katika maeneo mbalimbali kama vile mabenki, majengo, mikopo, hati fungani na ununuzi wa hisa. Mfuko wa Hifadhi umeendelea kuwekeza kwenye maeneo mawili ambayo ni Fedha na Majengo kwenye eneo la fedha hadi Machi 2023, ZSSF imewekeza jumla ya **TZS 573.288 bilioni** na eneo la uwekezaji wa majengo hadi Machi 2023jumla ya **TZS. 208.891 bilioni** zimeekezwa. Thamani ya uwekezaji ya ZSSF imeongezeka kwa asilimia **16.12** kwa **TZS. 782.18 bilioni** ukilinganisha na uwekezaji robo ya tatu ya mwaka 2021/22 ya kiasi cha **TZS. 673.57 bilioni**. Ongezeko hilo linachangiwa na uwekezaji wa ziada uliofanywa katika kipindi hicho kutokana na ongezeko la michango na mapato ya uwekezaji.

***Shirika la Bima (ZIC)***

73. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bima la Zanzibar lilianzishwa mwezi wa June mwaka 1969 ni miongoni mwa Mashirika yanayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100 likiwa chini ya Afisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar. Kwa hivi sasa Shirika linafanya kazi zake chini ya Sheria ya Msajili wa Hazina namba 6 ya mwaka 2021.

74. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya Shirika yanatokana na vianzio vyake vya mauzo ya Bima pamoja na faida zinazotokana na Uwekezaji, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023, Shirika limefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS 30.1 bilioni** ya mauzo ya Bima ambayo ni sawa na asilimia 81% ya makadirio ya kukusanya **TZS 37 bilioni** katika kipindi cha tathmini. Vile vile Shirika limefanikiwa kupata jumla ya **TZS 503 milioni** ya mapato yanayotokana na Uwekezaji.

75. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Shirika kwa kipindi cha Julai-Machi 2023 yamegawika kama ifuatavyo: -

i. **TZS 5.1 bilioni** zilitumika kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa ofisi (Management Expenses) sawa na asilimia 71% ya makadirio ya matumizi katika kipindi cha tathmini ambayo ni **TZS 7.0 bilioni;**

ii. **TZS 4.2 bilioni** zimetumika katika kulipa madai mbalimbali ya wateja waliopata ajali na kutimiza matakwa ya Sheria za bima; na

iii. **TZS 2.6 bilioni** zimetumika pia kulipa ujira kwa Mawakala na Madalali wanaofanya biashara ya bima kwa niaba ya Shirika.

76. **Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kulipa gawio Serikalini kwa mujibu wa kiwango kilichowekwa baada ya kupatikana kwa faida katika kipindi cha Julai-Machi 2023 Shirika limetoa **TZS 300 milioni** kama gawio kwa Serikali.

## F. MASHIRIKIANO NA TAASISI NYENGINE

77. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango, imeendelea kushirikiana na Taasisi nyengine ambazo zinapelekea malengo ya Ofisi kutimia. Baadhi ya Taasisi hizo na shughuli walizofanya katika kipindi hichi ni pamoja na:

***Wizara ya Fedha na Mipango***

Ofisi imeimarisha mashirikiano na Wizara ya Fedha na Mipango katika kukamilisha shughuli mbali mbali ikiwemo, majadiliano ya upatikanaji wa fedha za kusaidia Bajeti ya Serikali (GBS), upatikanaji wa fedha za miradi mbali mbali ikiwemo ya Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Pemba, Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu mbali mbali ikiwemo ya barabara na bandari, ushiriki wa pamoja katika vikao mbali mbali vya kimataifa vikiwemo vya Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Ofisi imeshirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, kuendelea na majadiliano ya kutafuta utaratibu bora wa kutatua changamoto mbali mbali za kikodi na biashara ambazo wanakumbana nazo wananchi wa pande mbili za muungano.

***Benki Kuu ya Tanzania (BOT)***

Ofisi inashirikiana na Benki Kuu ya Tanzania katika kupanga na kutekeleza Sera za Fedha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ofisi imeshiriki vikao mbali mbali vya Kamati ya Benki ya Tanzania katika kufuatilia na kupitisha mikakati kadhaa ya Sera za Fedha za Kibajeti kwa upande wa Zanzibar. Benki Kuu ya Tanzania inashirikiana na Ofisi pamoja na Tume ya Mipango kufanya tathmini ya mwenendo wa hali ya uchumi na viashiria vyake kama vya mwenendo wa hali bei, ujazo wa fedha, viwango vya kubadilisha fedha za kigeni pamoja na hali ya matumizi ya Serikali kwa ujumla. Ripoti mbili za Sera ya Fedha zimetolewa katika kipindi hichi pamoja na Ripoti nane za kila mwezi za Tathmini ya Hali ya Uchumi na Ripoti Tatu za Tathmini na Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa Robo Tatu za Mwaka.

*Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC)*

Tume ya Pamoja ya Fedha (Joint Finance Commission – JFC) imeendelea kufanya tafiti mbali mbali zinazohusu mwenendo wa kifedha katika pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, JFC imefanya tafiti zinazohusu Majukumu, Mapato na Matumizi yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano katika Wizara, Idara na Taasisi zilizo chini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi nyengine zinahusiana na ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za mapato na matumizi yanayohusu utekelezaji wa shughuli za Muungano kwa kipindi cha kuanzia Mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023 pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa Makatibu Wakuu na Mawaziri wa SMT na SMZ kuhusu masuala ya JFC.

*Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)*

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ina majukumu, pamoja na mambo mengine kuratibu na kusimamia shughuli za bima katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2022/2023, TIRA imekamilisha na kutoa miongozo kwa biashara ya bima kidijitali, imetoa muongozo wa Bima ya Kiislamu (Takaful) ambapo Shirika la Bima la Zanzibar limeanzisha Kampuni Tanzu (ZIC Takaful) na tayari imeshapatiwa usajili. Katika kipindi hichi, TIRA imesajili Kampuni za Bima 15 na kufanya ukuwaji wa sekta ya bima kwa upande wa Zanzibar kufikia asilimia 195.

## G. MWELEKEO WA BAJETI YA OR-FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2023-2024

*Ukusanyaji wa Mapato*

78. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2023/2024, Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango inaomba kukusanya jumla ya **TZS 2.768 trilioni**. Makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia **11** ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya **TZS 2.498 trilioni** yaliyopangwa mwaka 2022/2023. Mapato hayo yamekadiriwa kukusanywa katika mafungu ya OR-Fedha na Mipango **F01 TZS 1.946 trilioni**, **F04 TZS 120.000 milioni** na **F05 TZS 821.936 bilioni.** Mchanganuo wa makusanyo hayo kwa mafungu kama ifuatavyo:-

*Makusanyo ya Fungu F01*

79. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango inasimamia makusanyo katika maeneo mawili (2), eneo la kwanza mapato ya kodi

ambayo mapato hayo yanakusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 inaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 675.601 bilioni**, na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa upande wa Zanzibar inaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 520.643 bilioni.**

**80. Mheshimiwa Spika,** eneo la pili ni mapato yasiyokuwa ya kodi ambayo Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inaombewa kuidhinishiwa kupatikana kwa **TZS 634.426 bilioni** ambazo (Misaada **TZS 106.634 bilioni**, Mikopo **TZS 527.551 bilioni** na Mfuko wa pamoja wa Wafadhili **TZS 240.900 milioni**), Gawio la Mashirika inaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 35 bilioni,** Mapato ya Uhamiaji inaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 75 bilioni**, Kodi ya Bohari inaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 1.065 bilioni.**

**81. Mheshimiwa Spika,** Mapato mengineyo yasiyokuwa ya kodi ambayo Vifaa vikongwe inaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 2.360 bilioni**, Mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Ununuzi na uondoaji wa Mali za Serikali (usajili wa Wazabuni, Ada ya mafunzo, Matangazo na Ada ya matumizi ya nyaraka) inaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 750 milioni,** Ada ya ukodishwaji wa ukumbi inaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 22.830 milioni** na kodi ya Majengo ya Serikali inaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 913.199 milioni.**

***Makusanyo ya Fungu F04***

**82. Mheshimiwa Spika,** Makusanyo ya Fungu **F04** ni makusanyo yanayosimamiwa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 inaombewa kuidhinishiwa kukuasanya **TZS 64.750 milioni** kwa ajili ya mapato ya utafiti, **TZS 20 milioni** Mapato ya Washauri Elekezi na **TZS 35.250 milioni** Ada ya ukodishwaji wa Ukumbi.

***Makusanyo ya Fungu F05***

**83. Mheshimiwa Spika,** Makusanyo ya Fungu F05 ni makusanyo yanayosimamiwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 makusanyo ya Uhamisho wa Mapato ya Wafanyakazi (payee) yanaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 21 bilioni,** Misaada ya Kibajeti (GBS)-SMT inaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 52.190 bilioni,** Hati Fungani inaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 150 bilioni,** Mkopo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo inaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 567.210 bilioni,** Gawio la

Benki Kuu linaombewa kuidhinishiwa kupatikanwa kwa **TZS 13.500 bilioni**, Mabuku ya Stakabadhi yanaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 35.973 milioni** na Mchango kutoka Taasisi za Serikali unaombewa kuidhinishiwa kukusanya **TZS 18 bilioni**.

***Mchanganuo wa mapato yanaonekana katika kiambatisho Namba 3***

***Matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo***

**84.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023-2024, OR-Fedha na Mipango inakadiriwa kutumia jumla ya **TZS 682.879 bilioni** kwa mafungu yanayosimamiwa na OR-Fedha na Mipango, Uchambuzi wa matumizi ya Mafungu yake sita ni kama ifuatavyo: -

i. **Fungu F01** imekadiriwa kutumia **TZS 388.773 bilioni;**
ii. **Fungu F02** imekadiriwa kutumia **TZS 258.449 bilioni;**
iii. **Fungu F03** imekadiriwa kutumia **TZS 11.167 bilioni;**
iv. **Fungu F04** imekadiriwa kutumia **TZS 8.266 bilioni;**
v. **Fungu F05** imekadiriwa kutumia **TZS 11.142 bilioni na**
vi. **Fungu F06** imekadiriwa kutumia **TZS 5.082 bilioni**.

**85.** **Mheshimiwa Spika,** kutokana na taarifa hizo za mafungu naomba kuwasilisha uchambuzi wa matumizi ya Ofisi ya Raisi-Fedha na Mipango kwa programu zifuatazo:-

**Matumizi kwa fungu F01 yanakadiriwa kufikia TZS 388.773 bilioni** ambazo zitatumika katika utekelezaji wa programu kuu tatu (3).

**a. Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma**

**86.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **TZS 126.704 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 87.423 bilioni** ni mishahara iliyojumuisha (**TZS 86.087 bilioni** Marekebisho ya Mshahara na **TZS 1.336 bilioni** malipo ya Mshahara ya watendaji); **TZS 36.972 bilioni** fedha za Ruzuku kutoka Taasisi zinazosimamiwa na OR-Fedha na Mipango ambapo **(**Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) **TZS 21.328 bilioni** na Mfuko wa Barabara (ZRF) **TZS 15.644 bilioni)**; **TZS 350 milioni** Fedha za Mradi wa Kuhamasisha Uwezo kwa ajili ya Maendeleo, Fedha hizo ni ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (UNDP) na **TZS 1.959 bilioni** Fedha za utekelezaji wa shughuli za Ofisi. Mchanganuo wa Fedha kwa programu ndogo nne kama ifuatavyo: -

i. Usimamizi wa Bajeti ya Serikali **TZS 87.178 bilioni**;
ii. Uratibu wa Rasilimali za Nje **TZS 981.452 milioni**;
iii. Kusimamia Sera za Kodi na Fedha **TZS 37.891 bilioni**; na
iv. Usimamizi wa Mifumo ya Udhibiti wa Fedha za Umma **TZS 652.953 milioni.**

**b. Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma**

**87.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **TZS 80.416 bilioni** kati ya Fedha hizo **TZS 552.068 milioni** malipo ya Mishahara; **TZS 2.5 bilioni** Fedha za Hisa za ZPDC; **TZS 19.044 bilioni** Fedha za Mradi wa ujenzi wa Ofisi za Serikali; **TZS 55.078 bilioni** Mradi wa Ujenzi wa Mji Mpya wa Serikali; **TZS 2.617 bilioni** Fedha za Ruzuku ya ZPPDA; na **TZS 625.450 milioni** ni Fedha za utekelezaji wa shughuli za Ofisi. Mchanganuo wa Fedha kwa programu ndogo mbili kama ifuatavyo: -

i. Usimamizi ya Mitaji wa Umma **TZS 80.218 bilioni**; na
ii. Usimamizi wa Ununuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali **TZS 198.350 milioni.**

**c. Uendeshaji na Uratibu wa OR-Fedha na Mipango**

**88.** **Mheshimiwa Spika**, Programu hii inaombewa idhini ya kutumia **TZS 181.652 bilioni** kati ya fedha hizo **TZS 2.631 bilioni** malipo ya Mishahara; **TZS 144.000 bilioni** ni Mfuko wa Ulipaji wa Madeni; **TZS 1.754 bilioni** Fedha za Mradi wa Uimarishaji Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Mali Asili (ISP-DRM) ambazo ni mkopo nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika **(AfDB)** pamoja na Fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; **TZS 3.869 bilioni** Fedha za Mradi wa Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP); **TZS 22.810 bilioni** Fedha za Progamu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi (BIG-Z) ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia na **TZS 6.588 bilioni** ambazo ni fedha za utekelezaji wa shughuli za Ofisi kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mchanganuo wa programu ndogo tatu ni kama ifuatavyo: -

i. Utawala na Uendeshaji wa Wizara **TZS 5.715 bilioni;**
ii. Mipango, Sera na Utafiti wa Sekta ya Fedha **TZS 173.390 bilioni**; na
iii. Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi Pemba **TZS 2.547 bilioni.**

**Matumizi kwa fungu F02 yanakadiriwa kufikia TZS 258.449 bilioni** ambazo zitatumika kwa ajili ya kutekeleza Programu kuu moja.

**a. Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali**

89. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **TZS 258.449 bilioni** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. **TZS 2.449 bilioni** Fedha kwa ajili ya Mishahara;

ii. **TZS 25.000 bilioni** Malipo ya Mafao ya Kiinua Mgongo kwa wastaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

iii. **TZS 92.005 bilioni** Kulipa Riba na Mikopo inayoiva 2022/2023;

iv. **TZS 43.200 bilioni** Malipo ya Pencheni ya wastaafu;

v. **TZS 20.00 bilioni** Malipo ya Pencheni jamii; na

vi**. TZS 75.795 bilioni** Kulipa matumizi mengineyo maalumu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Matumizi kwa fungu F03 yanakadiriwa kufikia TZS 11.167 bilioni** ambazo zitatumika kutekeleza programu kuu tatu zifuatazo: -

**a.Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watenda Kazi**

90. **Mheshimiwa Spika**; Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **TZS 7.76 bilioni.** Kati ya Fedha hizo **TZS 689.044 milioni** malipo ya Mshahara**, TZS 2.500 bilioni** kwa ajili ya Programu ya Urasimishaji wa Ardhi na Biashara Zanzibar, lengo la Programu hii ni kuwakwamua wananchi na umasikini kupitia urasimishaji wa ardhi na biashara ili ziweze kutumika katika juhudi za kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Fedha hizi ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**, TZS 2.000 bilioni** kwa ajili ya Mradi wa Kuimarisha Ufanisi katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa Zanzibar, **TZS 1.500 bilioni** Mradi wa Usimamizi wa Upembuzi yakinifu wa Programu na Miradi ya Maendeleo lengo la mradi kuimarisha uandaaji na utayarishaji wa ripoti za upembuzi yakinifu kwa program na miradi ya maendeleo Fedha hizi ni Mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na **TZS 1.070 bilioni** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi. Mchanganuo wa fedha kwa programu ndogo tatu kama ifuatavyo: -

i. Uratibu wa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini **TZS 4.419 bilioni**;

ii. Maendeleo ya Watendakazi na Masuala ya Idadi ya Watu **TZS 871.207 milioni**; na

iii. Tathmini na Ufuatiliaji wa Mipango ya Maendeleo **TZS 2.470 bilioni**.

**b. Usimamizi wa Uchumi Mkuu**

**91. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **TZS 1.370 bilioni** kati ya Fedha hizo **TZS 391.658 milioni** malipo ya Mishahara; na **TZS 978.626 milioni** ni Fedha za utekelezaji wa shughuli za Ofisi. Mchanganuo wa Fedha kwa programu ndogo mbili kama ifuatavyo: -

i. Usimamizi wa Uchumi **TZS 405.960 milioni;** na

ii. Utafiti na Ubunifu **TZS 964.324 milioni.**

**c. Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango Zanzibar.**

**92. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya **TZS 2.036 bilioni** kati ya Fedha hizo **TZS 728.490 milioni** malipo ya Mishahara; na **TZS 1.308 bilioni** Fedha za utekelezaji wa shughuli za Ofisi. Mchanganuo programu ndogo mbili ni kama ifuatavyo: -

i. Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango Unguja **TZS 1.611 bilioni;** na

ii. Uratibu na Utekelezaji wa Tume ya Mipango Pemba **TZS 426.108 milioni**.

**Matumizi kwa fungu (F04) Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali TZS 8.266 bilioni ambazo zinatarajiwa kutekelezwa katika Programu kuu mbili zifuatazo: -**

**93. Mheshimiwa Spika**; Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **TZS 8.266 bilioni** kati ya Fedha hizo **TZS 2.219 bilioni** malipo ya Mshahara**; TZS 4.427 bilioni** Fedha za Mkopo kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II) lengo la mradi kuimarisha shughuli za kitakwimu Zanzibar hususani kuwezesha ukusanyaji, upatikanaji na utoaji wa takwimu za kawaida chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia na **TZS 1.619 bilioni** Fedha za utekelezaji wa shughuli za Ofisi. Mchanganuo wa Fedha kwa programu ndogo nne kama ifuatavyo: -

i. Kuendeleza na Kuratibu Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii **TZS 5.97 bilioni;**
ii. Uratibu wa shughuli za kitakwimu katika Mfumo wa taifa wa Takwimu **TZS 1.217;**
iii. Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali **TZS 1.659 bilioni; na**
iv. Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Takwimu Pemba **TZS 631 milioni.**

**Matumizi kwa fungu F05 yanakadiriwa kufikia TZS 11.142 bilioni ambazo zitatumika kutekeleza programu kuu mbili (2)**

**a. Usimamizi wa Hazina**

94. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **TZS 664.30 milioni** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi. Mchanganuo wa Fedha kwa programu ndogo nne kama ifuatavyo: -

i. Usimamizi wa Mapato ya Serikali yasiyokua ya Kodi **TZS 111.180 milioni**;
ii. Kusimamia Ufungaji wa Hesabu Jumuishi za Serikali **TZS 46.440 milioni**;
iii. Usimamizi wa Matumizi ya Serikali **TZS 143.145 milioni**; na
iv. Usimamizi wa Deni la Taifa na Huduma za Mfuko Mkuu **TZS 363.535 milioni.**

**b. Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

95. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa idhini ya kutumia **TZS 10.478 bilioni** kati ya Fedha hizo **TZS 8.93 bilioni** malipo ya Mishahara na **TZS 1.548 bilioni** Fedha za utekelezaji wa shughuli za Ofisi. Mchanganuo programu ndogo tatu ni kama ifuatavyo: -

i. Utawala na Uendeshaji Unguja **TZS 7.929 bilioni**;
ii. Utawala na Uendeshaji Pemba **TZS 2.214 bilioni**; na
iii. Uratibu Mipango na Sera **TZS 335.63 milioni.**

**Matumizi kwa fungu (F06) Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali inakadiriwa kufikia TZS 5.082 bilioni ambazo zitatumika katika kutekeleza programu kuu mbili (2) zifuatazo: -**

**a. Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani wa Serikali**

96. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **TZS 210.617 milioni** kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Ofisi. Mchanganuo wa Fedha kwa programu ndogo tatu kama ifuatavyo:-

i. Usimamizi wa Kamati za Ukaguzi na Taarifa Jumuishi za Ukaguzi wa Ndani **TZS 63.832 milioni**;

ii. Uchunguzi wa Ubadhirifu na vihatarishi **TZS 121.275 milioni**; na

iii. Usimamizi wa Uthibitisho wa Ubora **TZS 25.510 milioni**.

**b. Utawala na Uendeshaji**

97. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inaombewa kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **TZS 4.871 bilioni** kati ya Fedha hizo **TZS 3.677 bilioni** malipo ya Mshahara (Unguja **TZS 2.969 bilioni** na Pemba **TZS 707.616 milioni**); **TZS 1.194 bilioni** Fedha za utekelezaji wa shughuli za Ofisi. Mchanganuo wa Fedha kwa programu ndogo mbili (2) kama ifuatavyo:-

i. Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mipango, Mafunzo na Utafiti **TZS 4.068 bilioni**; na

ii. Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi Pemba TZS **803.201 milioni**.

## H. MWELEKEO WA KAZI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA OR-FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2023/2024

***Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)***

98. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ni Wakala Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika ukusanyaji wa mapato kwa vianzio vya ndani. ZRA inakusanya mapato kutokana na vianzio mbali mbali vya ndani. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ZRA imekadiriwa kukusanya Jumla ya **TZS 675.601 bilioni.** Makadirio haya ni sawa na ongezeko la **TZS 66.099 bilioni** sawa na asilimia **17** ya makadirio ya makusanyo ya vianzio vya kodi kwa mwaka 2022/2023. Ili kufikia au kuvuka lengo lililowekwa, ZRA inatarajia:-

i. Kuimarisha Mifumo ya Ukusanyaji wa Kodi, ikiwemo Kuanza Matumizi ya MFUMO MPYA wa Usimamizi wa Ukusanyaji Mapato ya Kodi (ZIDRAS- Zanzibar Integrated Domestic Revenue Administration System);

ii. Kuendelea kuimarisha huduma za kikodi kupitia ofisi zake za Mikoa ya Kodi;
iii. Kuendelea kutumia Mifumo katika Ukusanyaji wa kodi kwa kusajili walipakodi 3,000 wapya katika mfumo wa kutolea risiti za kielektroniki wa VFMS;
iv. Kuendelea kujenga uweledi na uadilifu kwa wafanyakazi wa ZRA;
v. Kuendelea kuongeza uwajibikaji wa hiari wa walipa kodi, Kufanya ukaguzi wa kina katika sekta za Utalii, Mawasiliano na Taasisi za kifedha;
vi. Kuanzisha kitengo cha "Business Intelligent Unit" ambacho kitahusika kufanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali za walipakodi; na
vii. Kutanua wigo wa kodi kwa kusajili walipakodi wapya 6,000 Unguja na Pemba.

99. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mamlaka ya Mapato Zanzibar imepangiwa kutumia Jumla ya **TZS 28.56 bilioni** kwa shughuli za kawaida na shughuli za maendeleo. Mamlaka ya Mapato Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 itatekeleza bajeti yake kupitia programu kuu mbili, Programu ya Ukusanyaji Mapato ya Serikali kwa Ufanisi na Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za ZRA.

***Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)***

100. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Tanzania Ofisi ya Zanzibar inaendelea na kazi ya uwakala wa Serikali wa kukusanya mapato yatokanayo na vianzio mbali mbali vya kodi. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, imekadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 520.643 bilioni**. Ambapo Idara ya Forodha inatarajiwa kukusanya **TZS 257.340 bilioni** na Idara ya Kodi za Ndani **TZS 263.303 bilioni**.

***Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)***

101. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ inatarajia kuongeza mapato ya benki kwa asilimia 19 kutoka **TZS 121 bilioni** na kufikia **TZS 144.36 bilioni** kutokana na mapato ya mikopo, mapato mengine yasiyo ya riba na uwekezaji mbali mbali. Kuongeza matumizi kwa asilimia 19 na kufikia **TZS 92.53 bilioni** kutoka **TZS 77.5 bilioni** kutokana na kufunguliwa kwa matawi Tanzania Bara na vituo vya kutolea huduma Zanzibar.

102. **Mheshimiwa Spika,** PBZ inatarajia kuongeza mikopo kwa asilimia 17 hadi kufikia **TZS 941 bilioni** kutoka **TZS 802 bilioni**, ongezeko hilo litatokana na mikopo ya wafanyakazi wa sekta ya umma Zanzibar pamoja na Tanzania Bara ambapo benki inategemea kufungua matawi zaidi. Kuongezeka kwa rasilimali za benki kwa asilimia 19 na kufikia **TZS 1,661.79 bilioni** kutoka **TZS 1,402 bilioni.** Aidha, Benki inakadiria ongezeko la ukusanyaji wa amana za wateja kwa asilimia 36 na kufikia **TZS 1,443.53 bilioni** kutoka **TZS 1,063 bilioni.**

103. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa miradi, PBZ inatarajia kutekeleza miradi ifuatayo kwa mwaka 2023: -

i. Kuendelea na mchakato wa uanzishwaji wa matawi mapya ya benki katika mikoa ya Mbeya na Morogoro;

ii. Ujenzi wa vituo vya kutolea huduma katika maeneo ya Nungwi, Konde, na Uwanja wa Ndege *Terminal 3* pamoja na eneo la Amani;

iii. Kufanya upembuzi yakinifu katika mikoa ya Tanga, Mwanza na Arusha ili kuweza kufungua huduma za kibenki katika maeneo hayo;

iv. Kuongeza mawakala 1,000 ili kutekeleza azma ya benki kuwafikishia huduma wateja wake karibu na makazi yao;

v. Kujenga jengo la kuhifadhia nyaraka za Benki katika eneo la Mwanakwerekwe Unguja;

vi. Kununua mashine mpya kumi na moja (11) za kutolea fedha ambazo nyengine zitawekwa katika maeneo mapya na nyengine zitatumika kuzibadilisha ATM ambazo zimekuwa kongwe na hazifanyi kazi vizuri;

vii. Kuboresha mifumo ya benki ikiwemo kununua switch ambayo itarahisisha na kuboresha huduma za ATM kwa wateja; na

viii. Kufanya ukarabati mkubwa katika matawi ya Forodhani na Malindi.

***Mfuko wa Barabara (ZRF)***

104. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, ZRF imepangiwa **TZS 15.644 bilioni**. Kati ya fedha hizo **TZS 13.718 bilioni** zinatarajiwa kutumika kwa kazi mbali mbali ikiwa ni pamoja na kukamilisha barabara ya Kipapo-Mgelema-Wambaa na matengenezo makubwa ya barabara za Kisiwa cha Tumbatu, Kilombero-Mgonjoni, Kiboje-Uchukuni, Kinyasini-Bandamaji, Fuoni Maharibiko-Mshelishelini, Fuoni-Mtundani-Uwandani-Maungani kwa upande wa

Unguja na barabara za Chanjaani-Pujini, Mizingani-Wambaa, Kenya-Chambani, Mtambile-Kangani, Mtambile-Mwambe na Micheweni Msituni-Msasani kwa Pemba. **Mheshimiwa Spika,** kazi za uendeshaji wa Mfuko zimepangiwa **TZS 1.925 bilioni** kuendeleza uimarishaji wa ufanisi wa kazi na uwajibikaji katika kusimamia matumizi bora ya fedha.

***Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)***

**105. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) unatarajia kukusanya jumla ya **TZS 223.5 billioni** kutoka katika vyanzo vikuu viwili ambavyo ni michango ya wanachama na mapato ya uwekezaji. Mfuko unakadiria kukusanya jumla ya **TZS 148.6 bilioni** kutokana na michango ya wanachama na **TZS 74.9 bilioni** kama mapato ya uwekezaji. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, ZSSF inatarajia kufanya malipo ya mafao, uwekezaji na gharama za uendeshaji kwa **TZS 216.5 bilioni,** kati ya fedha hizo **TZS 13.7 billioni** kwa ajili ya gharama za uendesahaji, **TZS 71.1 billioni** kwa ajili ya Mafao na **TZS 131.7 billioni** kwa ajili ya uwekezaji.

**106. Mheshimiwa Spika,** ZSSF itaendelea na uwekezaji endelevu wa majengo ikiwemo:

i. Kuendelea na hatua za ujenzi wa kituo cha kisasa cha mabasi cha Kijangwani ambazo zinatarajia kuanza baada ya makubaliano baina ya Mfuko na Kampuni ya CRJE (EA) LTD;

ii. Kuendelea na mradi wa ujenzi wa jengo la maegesho ya gari Malindi baada ya makubaliano baina ya Mfuko na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM);

iii. Kuendelea na hatua za ujenzi wa mradi wa Nyumba za Bei Nafuu ambayo majengo yanaendela kujengwa na kampuni ya CRJE; na

iv. Kukamilisha hatua za kumtafuta mkandarasi zinakamilika na kuendelea na hatua za ujenzi wa eneo la Michezo na Biashara Mbweni.

***Shirika la Bima Zanzibar (ZIC)***

**107. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bima kwa mwaka fedha 2023/2024 linatarajia kukusanya jumla ya **TZS 59.5 bilioni** kutoka katika vianzio vyake vya mapato ya biashara ya Bima na **TZS 940 milioni** mapato yanayotokana na Uwekezaji. Hivyo, katika kuweza kufikia ukusanyaji wa mapato hayo Shirika limejipangia kutekeleza mikakati ifuatayo: -

i. Kutoa taaluma kwa Wananchi na Taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi juu ya suala la kujiwekea kinga mali zao kwa lengo la kuongeza idadi ya wateja wapya na biashara mpya zisizokuwa za magari katika mtandao wake;

ii. Kutambulisha na kuanzisha bidhaa mpya katika soko la bima zinazokidhi mahitaji ya jamii, bidha hizo ni kama zifuatazo: - Bima ya Wasafiri, Bima ya Waendesha Watalii, Bima ya Wasafirishaji, Bima ya Maisha "Life Assurance" na Bima ya ajali kwa Madereva;

iii. Kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha Miradi yote mikubwa ya Maendeleo kwa Wananchi inakatiwa kinga za Bima na Shirika; na

iv. Shirika kuendelea na mikakati ya kuwafuatilia wateja wake kwa zaidi ya asilimia 80 (Customer Retention).

108. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, Shirika kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 limepanga kutumia jumla ya **TZS 23 bilioni** ikijumuisha matumizi yafuatayo:-

i. Matumizi kwa kazi za uendeshaji za Shirika "Management Expenses" **TZS 15.3 bilioni;**

ii. Matumizi ya ununuzi wa vitendea kazi pamoja na ununuzi wa vifaa mbali mbali vya ICT ni **TZS 1.8 bilioni;**

iii. Ununuzi wa magari mawili kwa matumizi ya Shirika ni **TZS 260 milioni;**

iv **TZS 5.0** bilioni zikiwa ni ununuzi wa Jengo kwa matumizi ya ofisi Pamoja na ukodishaji kwa upande wa Tanzania Bara kanda ya Pwani Dar es salaam; na

v. Vilevile **TZS 700** milioni zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya gharama za kuyafanyia marekebisho na ukarabati "Renovation" kwa majengo yote yanayomilikiwa na Shirika.

***Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA)***

109. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA), kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 imekadiria kukusanya **TZS 750 milioni** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato. Kwa upande wa matumizi ZPPDA, inaomba kuidhinishiwa jumla ya **TZS 2.617 bilioni** ambayo ni ruzuku kutoka Serikalini kati ya Fedha hizo **TZS 1.579 bilioni** kwa ajili ya ulipaji wa mishahara na **TZS**

**1.038 bilioni** kwa kutekeleza shughuli za ofisi. Mamlaka itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016 kama ifuatavyo:-

i. Kufanya ukaguzi na uchunguzi wa ununuzi na uondoaji wa mali za Umma katika Taasisi za Umma 36;

ii. Kutoa mafunzo ya sheria ya ununuzi, Kanuni na miongozo kwa maafisa manunuzi 120, maafisa masuali 18, wajumbe wa bodi ya zabuni 200;

iii. Kufanya mafunzo kwa wazabuni juu ya kujaza vitabu vya zabuni na usajili katika mfumo wa ununuzi washiriki 280;

iv. Kufanya mafunzo juu ya miongozo mbali mbali kwa Taasisi nunuzi na wadau wa ununuzi 100;

v. Kuandaa miongozo na nyaraka za ununuzi;

vi. Kufanya mkutano mkuu wa ununuzi wa mwaka kwa watoa huduma 280;

vii. Kutengeneza vipindi vitatu vya radio na tv kuhusiana na majukumu ya Mamlaka; na

viii. Kufanya vikao kwa Taasisi nunuzi, Idara Maalumu za SMZ na Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka.

## I. SHUKRANI

**110. Mheshimiwa Spika,** Matayarisho ya Bajeti yamehusisha wadau wengi, wakiwemo watendaji wa Ofisi yetu na taasisi mbali mbali ambao tumeshirikiana kukamilisha kazi hii. Naomba kutoa shukrani za dhati kwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango Mheshimiwa Ali Suleiman Mrembo na wafanyakazi wa Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Juma Malik Akil, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Dkt. Rahma Salum Mahfoudh, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango Nd. Aboud Hassan Mwinyi, Mhasibu Mkuu wa Serikali Dkt. Said Seif Mzee, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani Ndugu Fatma Khamis Mohammed pamoja na Wakuu wa Idara zote za Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango wakiwemo Makamishna na Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi chini ya Ofisi na Maafisa wote kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha kuwa majukumu ya Ofisi yanatekelezwa kwa ufanisi.

## J. HITIMISHO

111. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya taarifa hiyo, naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kupokea, kujadili na hatimae kuikubali taarifa ya utekelezaji ya kipindi cha Julai-Machi 2023 na kuidhinisha makadirio ya mapato ya **TZS 2.768 trilioni** na matumizi ya kawaida na maendeleo ya **TZS 682.879 bilioni** ya OR-Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

112. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

.......................................

**DKT: SAADA MKUYA SALUM,**
**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO.**

# VIAMBATISHO

**KIAMBATANISHO NO 1**

## OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO
## MUHTASARI WA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI -MACHI, 2022/2023

| VIAZIO | MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023 | MAKADIRIO JULAI - MACHI,2022/23 | HALISI JULAI - MACHI,2022/23 | ASILIMIA JULAI- MACHI 2022/23 |
|---|---|---|---|---|
| **MAPATO FO1** | | | | |
| **MAPATO YA KODI** | | | | |
| MAMLAKA YA MAPATO (TRA) | 454,056,841,000 | 337,048,358,510 | 325,611,880,000 | 97 |
| ZRA | 579,502,183,000 | 460,500,912,377 | 449,283,026,860 | 98 |
| **JUMLA NDOGO** | **1,033,559,024,000** | **797,549,270,887** | **774,894,906,860** | **97** |
| MIKOPO NA MISAADA KUTOKA KWA ODA | 677,964,901,000 | 508,473,675,750 | 112,831,290,151 | 22 |
| **JUMLA NDOGO** | **677,964,901,000** | **508,473,675,750** | **112,831,290,151** | **22** |
| **MAPATO YASIO KUWA YA KODI** | | | | |
| GAWIO LA MASHIRIKA | 20,000,000,000 | 20,000,000,000 | 6,618,485,083 | 33 |
| KODI YA BOHARI | 1,065,399,000 | 665,744,000 | 170,435,000 | 26 |
| UHAMIAJI | 56,597,600,000 | 56,597,600,000 | 60,507,315,068 | 107 |
| **JUMLA NDOGO** | **77,662,999,000** | **77,263,344,000** | **67,296,235,151** | **87** |
| **MAPATO MENGINEYO YASIYOKUWA YA KODI** | | | | |
| SALES OF ABSOLETE STORES(VIFAA VIKONGWE) | 1,902,498,000 | 2,029,236,000 | 920,866,750 | 45 |
| USAJILI WA WAZABUNI NA NYARAKA ZA ZABUNI | 684,900,000 | 391,482,000 | 323,863,998 | 83 |
| NYARAKA ZA ZABUNI | 22,830,000 | 20,754,540 | | |
| RENT FOR BUILDING | 913,199,000 | 480,000,000 | 213,784,000 | 45 |
| COUNTER FOIL(MABUKU NA STAKABADHI) | 15,220,000 | 13,339,970 | 6,420,000 | 48 |
| ADA YA UKODISHWAJI UKUMBI | 22,830,000 | 28,259,954 | 8,700,000 | 31 |
| **JUMLA NDOGO** | **3,561,477,000** | **2,963,072,464** | **1,473,634,748** | **50** |
| **JUMLA FO1** | **1,792,748,401,000** | **1,386,249,363,101** | **956,496,066,910** | **69** |
| **MAPATO FO4** | | | | |
| MAPATO YA UTAFITI | 185,000,000 | 138,000,000 | 39,810,271 | **29** |
| **JUMLA NDOGO** | **185,000,000** | **138,000,000** | **39,810,271** | **29** |
| **MAPATO FO5** | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UHAMISHO WA MAPATO YA WAFANYAKAZI (PAYE) | 21,000,000,000 | 15,750,000,000 | 14,000,000,000 | 89 |
| MCHANGO MAMLAKA(ZURA) | 6,000,000,000 | 4,500,000,000 | 4,500,000,000 | 100 |
| MABUKU NA STAKABADHI | 45,673,000 | 34,283,000 | 12,449,000 | 36 |
| MCHANGO BODI YA WASANIFU | 662,069,000 | 521,388,000 | 254,212,050 | 49 |
| MCHANGO BODI YA WAKANDARASI | 1,445,899,000 | 1,023,996,300 | 420,865,500 | 41 |
| HATI FUNGANI | 115,000,000,000 | | | |
| MKOPO KWA AJILI YA MIRADI YA MAENDELEO | 400,000,000,000 | 250,000,000,000 | 27,000,000,000 | 11 |
| GAWIO LA BOT | 12,000,000,000 | | | |
| MCHANGO BODI YA UHALISHAJI ARDHI | 3,424,497,000 | 2,555,669,500 | 539,937,850 | 21 |
| MAREJESHO YA MKOPO | 135,700,000,000 | | | |
| MISAADA YA KIBAJETI (GBS/URT) | 10,000,000,000 | 10,000,000,000 | 67,435,026,427 | 674 |
| **JUMLA NDOGO** | **705,278,138,000** | **284,385,336,800** | **114,162,490,827** | **40** |
| **JUMLA KUU** | **2,498,211,539,000** | **1,670,772,699,901** | **1,070,698,368,007** | **64** |

**KIAMBATISHO NO. 2**

**MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO JULAI -MACHI, 2022/2023**

| Programu Kuu | Programu ndogo | Makisio Mwaka (2022-2023) | Makisio Julai-Mach 2022-2023 | Mishahara | Matumizi ya Mengineyo | Maendeleo | | Ruzuku | Jumla | Asilimia ya Fedha zilizopatikana kwa Julai-Mach |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Tarakimu ni milioni | | | | SMZ | Mhisani | | | |
| Bajeti na Usimamizi wa Fedha za Umma | Usimamizi wa Bajeti ya Serikali | 179,276.405 | 1,136.409 | 502.546 | 87.667 | | 84.694 | | 674.907 | 59% |
| | Uratibu wa Fedha za Nje | 430.894 | 341.849 | 199.276 | 138.845 | | | | 338.121 | 99% |
| | Fedha na Sera za Kodi | 53,825.931 | 25,272.591 | 257.417 | 76.728 | | | 18,707.800 | 19,041.945 | 75% |
| | Usimamizi wa mifumo ya udhibiti na usimamizi wa fedha za umma | 963.216 | 1,746.861 | | 1,256.044 | | | | 1,256.044 | 72% |
| | **Jumla ndogo** | **234,496.45** | **28,497.710** | **959.239** | **1,559.284** | | **84.694** | **18,707.800** | **21,311.017** | **75%** |
| Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma | Mitaji ya Umma | 106,779.769 | 12,053.878 | 499.363 | 1,577.786 | 817.183 | | 1,250.454 | 4,144.786 | 34% |
| | Usimamizi wa ununuzi na Uhakiki wa Mali za Serikali | 745.138 | 326.730 | | 40.000 | | | | 40.000 | 12% |
| | **Jumla ndogo** | **107,524.91** | **12,380.61** | **499.363** | **1,617.786** | **817.183** | | **1,250.454** | **4,184.786** | **34%** |
| Uendeshaji na uratibu wa wizara ya Fedha na Mipango | Utumishi na Uendeshaji | 4,326.880 | 4,964.411 | 1,368.376 | 2,120.597 | | | | 3,488.973 | 70% |
| | Mipango, Sera na Utafiti | 51,797.320 | 2,136.433 | 137.134 | 88.501 | | 1,488.785 | | 1,714.420 | 80% |
| | Ofisi kuu Pemba | 3,224.845 | 1,914.801 | 583.481 | 446.884 | | | | 1,030.365 | 54% |
| | **Jumla ndogo** | **59,349.05** | **9,015.65** | **2,088.99** | **2,655.98** | | **1,488.79** | | **6,233.758** | 69% |
| | **Jumla F01** | **401,370.40** | **49,893.96** | **3,547.593** | **5,833.052** | **817.183** | **1,573.479** | **19,958.254** | **31,729.561** | **64%** |
| Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | 211,604.800 | 138,342.000 | 119,478.000 | | | | | 119,478.000 | **86%** |
| | **Jumla ndogo** | **211,604.80** | **138,342.000** | **119,478.000** | | | | | **119,478.00** | 86% |
| | **Jumla F02** | **211,604.80** | **138,342.000** | **119,478.000** | | | | | **119,478.000** | **86%** |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya watendakazi | Uratibu wa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umaskini | 12,872.158 | 11,541.680 | 154.276 | 70.846 | | 307.113 | | 532.235 | 5% |
| | Maendeleo ya Watendakazi wa Masuala ya Idadi ya Watu | 901.353 | 722.653 | 153.383 | 153.481 | | | | 306.864 | 42% |
| | Tathmini na Ufuatiliaji wa Mipango ya Maendeleo | 1,153.631 | 956.691 | 239.960 | 67.632 | | | | 307.592 | 32% |
| | **Jumla ndogo** | **14,927.14** | **13,221.02** | **547.62** | **291.96** | | **307.11** | | **1,146.69** | 9% |
| Usimamizi wa Uchumi Mkuu | Usimamizi wa Uchumi Mkuu | 579.395 | 393.862 | 151.049 | 75.842 | | | | 226.891 | 58% |
| | Utafiti | 933.93 | 807.269 | 115.614 | 138.286 | | | | 253.900 | 31% |
| | **Jumla ndogo** | **1,513.32** | **1,201.13** | **266.66** | **214.13** | | | | **480.791** | 40% |
| Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango | Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango | 2,012.409 | 1,639.071 | 393.092 | 764.569 | | | | 1,157.661 | 71% |
| | Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango Pemba | 484.31 | 363.228 | 166.695 | 67.000 | | | | 233.695 | 64% |
| | **Jumla ndogo** | **2,496.71** | **2,002.30** | **559.79** | **831.57** | | | | **1,391.36** | **69%** |
| | **Jumla F03** | **18,937.18** | **16,424.45** | **1,374.07** | **1,337.66** | | **307.11** | | **3,018.838** | **18%** |
| Kuendeleza na kuratibu Takwimu rasmi za kiuchumi na kijamii | Ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa Takwimu Rasmi za Kiuchumi na Kijamii | 10,793.368 | 9,434.063 | | 109.031 | | 7,095.85 | | 7,204.882 | **76%** |
| | Uratibu wa shughuli za Kitakwimu katika mfumo wa Taifa wa Takwimu Zanzibar | 1,979.467 | 99.759 | | 48.751 | | | | 48.751 | **49%** |
| | **Jumla ndogo** | **12,772.835** | **9,533.822** | | **157.782** | | **7,095.85** | | **7,253.633** | **76%** |
| uendeshaji na uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | Utawala na Uendeshaji Unguja | 3,769.499 | 2,129.986 | 1,675.959 | 304.802 | | | | 1,980.761 | 93 |
| | Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Takwimu Pemba | 512.835 | 176.025 | | 54.107 | | | | 54.107 | 31 |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jumla ndogo** | **4,282.334** | **2,306.011** | **1,675.959** | **358.909** | | | | **2,034.868** | **88** |
| | **Jumla F04** | **17,055.169** | **11,839.833** | **1,675.959** | **516.691** | | **7,095.851** | | **9,288.501** | **78** |
| Usimammizi wa Hazina | Ufuatiliaji wa Mapato ya Serikali yasiyokuwa ya Kodi | 108.975 | 88.266 | | 22.580 | | | | 22.580 | 26 |
| | Kusimamia ufungaji wa Hesabu Jumuishi za Serikali | 220.120 | 171.590 | | 35.620 | | | | 35.620 | 21 |
| | Usimamizi wa Matumizi ya Serikali | 570.370 | 385.247 | | 183.682 | | | | 183.682 | 48 |
| | **Jumla ndogo** | **899.465** | **645.103** | | **241.882** | | | | **241.882** | 37 |
| Uendeshaji na uratibu wa Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | Utawala na Uendeshaji Unguja | 5,327.109 | 5,891.519 | 4,988.137 | 418.670 | | | | 5,406.807 | 92 |
| | Utawala na Uendeshaji Pemba | 1,259.326 | 1,610.987 | 1,296.489 | 89.078 | | | | 1,385.567 | 86 |
| | **Jumla ndogo** | **6,586.435** | **7,502.506** | **6,284.626** | **507.748** | | | | **6,792.374** | **91** |
| | **Jumla F05** | **7,485.900** | **8,147.609** | **6,284.626** | **749.630** | | | | **7,034.256** | **86** |
| Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali | Usimamizi wa kamati za Ukaguzi na Taarifa jumuishi za ukaguzi wa ndani | 307.500 | 298.49 | | 130.91 | | | | 130.910 | 44 |
| | Uchunguzi wa Ubadhirifu na vihatarishi | 696.434 | 71.50 | | 13.04 | | | | 13.040 | 18 |
| | Usimamizi wa uthibitisho wa ubora | 134.540 | 539.87 | | 67.36 | | | | 67.360 | 12 |
| | **Jumla ndogo** | **1,138.474** | **909.860** | | **211.310** | | | | **211.310** | **23** |
| Utawala na Uendeshaji | Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mipango,Mafunzo na Utafiti | 1,876.051 | 2,303.36 | 2,056.00 | 133.50 | | | | 2,189.500 | 95 |
| | Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Ofisi Pemba | 623.175 | 539.68 | 490.16 | 19.41 | | | | 509.570 | 94 |
| | **Jumla ndogo** | **2,499.226** | **2,843.040** | **2,546.160** | **152.910** | | | | **2,699.070** | **95** |
| | **Jumla F06** | **3,637.700** | **3,752.900** | **2,546.160** | **364.220** | | | | **2,910.380** | **78** |
| | **JUMLA KUU F01+F02+F03+F04+F05 +F06** | **660,091.145** | **228,400.759** | **134,906.407** | **8,801.249** | **817.183** | **8,976.443** | **19,958.254** | **173,459.536** | **76** |

| KIAMBATANISHO NO 3 | | | |
|---|---|---|---|
| **OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO** | | | |
| **MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024** | | | |
| **VIAZIO** | **MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023** | **MAKADIRIO KWA MWAKA 2023/2024** | **TOFAUTI** |
| **MAPATO FO1** | | | |
| **MAPATO YA KODI** | | | |
| MAMLAKA YA MAPATO (TRA) | 454,056,841,000 | 520,643,979,000 | 66,587,138,000 |
| ZRA | 579,502,183,000 | 675,601,262,000 | 96,099,079,000 |
| **JUMLA NDOGO** | **1,033,559,024,000** | **1,196,245,241,000** | **162,686,217,000** |
| MIKOPO NA MISAADA KUTOKA KWA ODA | 677,964,901,000 | 634,426,588,000 | - 43,538,313,000 |
| **JUMLA NDOGO** | **677,964,901,000** | **634,426,588,000** | **- 43,538,313,000** |
| **MAPATO YASIO KUWA YA KODI** | | | |
| GAWIO LA MASHIRIKA | 20,000,000,000 | 35,000,000,000 | 15,000,000,000 |
| KODI YA BOHARI | 1,065,399,000 | 1,065,399,000 | - |
| UHAMIAJI | 56,597,600,000 | 75,000,000,000 | 18,402,400,000 |
| **JUMLA NDOGO** | **77,662,999,000** | **111,065,399,000** | **33,402,400,000** |
| **MAPATO MENGINEYO YASIYOKUWA YA KODI** | | | |
| SALES OF ABSOLETE STORES(VIFAA VIKONGWE) | 1,902,498,000 | 2,360,018,000 | 457,520,000 |
| USAJILI WA WAZABUNI NA NYARAKA ZA ZABUNI | 684,900,000 | 750,000,000 | 65,100,000 |
| NYARAKA ZA ZABUNI | 22,830,000 | | (22,830,000) |
| RENT FOR BUILDING | 913,199,000 | 913,199,000 | - |
| COUNTER FOIL(MABUKU NA STAKABADHI) | 15,220,000 | | (15,220,000) |
| ADA YA UKODISHWAJI UKUMBI | 22,830,000 | 22,830,000 | - |
| **JUMLA NDOGO** | **3,561,477,000** | **4,046,047,000** | **484,570,000** |
| **JUMLA FO1** | **1,792,748,401,000** | **1,945,783,275,000** | **153,034,874,000** |
| **MAPATO FO4** | | | |
| MAPATO YA WASHAURI ELEKEZI | | 20,000,000 | |
| ADA YA UKODISHWAJI UKUMBI | | 35,250,000 | |
| MAPATO YA UTAFITI | 185,000,000 | 64,750,000 | - 120,250,000 |
| **JUMLA NDOGO** | **185,000,000** | **120,000,000** | - 65,000,000 |
| **MAPATO FO5** | | | |
| UHAMISHO WA MAPATO YA WAFANYAKAZI (PAYE) | 21,000,000,000 | 21,000,000,000 | - |
| MCHANGO MAMLAKA(ZURA) | 6,000,000,000 | | |
| MABUKU NA STAKABADHI | 45,673,000 | 35,973,000 | - 9,700,000 |
| MCHANGO BODI YA WASANIFU | 662,069,000 | | |
| MCHANGO BODI YA WAKANDARASI | 1,445,899,000 | | |
| HATI FUNGANI | 115,000,000,000 | 150,000,000,000 | 35,000,000,000 |
| MKOPO KWA AJILI YA MIRADI YA MAENDELEO | 400,000,000,000 | 567,210,000,000 | 167,210,000,000 |
| GAWIO LA BOT | 12,000,000,000 | 13,500,000,000 | 1,500,000,000 |
| MCHANGO BODI YA UHALISHAJI ARDHI | 3,424,497,000 | | |
| MAREJESHO YA MKOPO | 135,700,000,000 | | |
| MCHANGO KUTOKA KWA TAASISI ZA SERIKALI | | 18,000,000,000 | |
| MISAADA YA KIBAJETI (GBS/URT) | 10,000,000,000 | 52,190,000,000 | 42,190,000,000 |
| **JUMLA NDOGO** | **705,278,138,000** | **821,935,973,000** | **116,657,835,000** |
| **JUMLA KUU** | **2,498,211,539,000** | **2,767,839,248,000** | **269,627,709,000** |
| | | | |